SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA
PAKUA SASA



## Serikali yaonya shule inayokataa wanafunzi wagonjwa


UKURASA 5



MAISHA
Nipashe Jumapili
Baba, Mama na Mwana



Faida za karoti ni hizi....



MAISHA NI NYUMBA
Kuwa mbunifu kupangilia nyumba ya nafasi ndogo



KATUNIKA



USO WENYE MAFUTA
Njia hizi zitakusaidia kujing'arisha


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Agosti 29, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580687

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


RIPOTI MAALUM

# Kilichojificha ndoa za 'babu na mjukuu'

**Zimo** pia za 'bibi na mjukuu'. Wataalamu, viongozi wa dini watoa angalizo... *Endelea ukurasa 4*



Alhad Mussa Salum



## Kizimkazi kupaisha utalii wa Tanzania

UKURASA 2

Rais Samia Suluhu Hassan, akipiga kofi baada ya kuzindua kliniki inayotembea iliyotolewa na Benki ya NBC kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), ili kuboresha huduma ya afya hususani ya mama na mtoto, wakati wa hafla katika Kijiji cha Kizimkazi Mkunguni, mkoani Kusini Unguja jana. Wengine ni Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee Jinsia na Watoto Zanzibar, Ahmed Mazrui (wa pili kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Theobald Sabi (wa tatu kushoto) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora wa SMZ, Haroun Ali Suleiman (kulia). **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

UKURASA WA 3

### MAJALIWA AJIVUNIA MABORESHO ELIMU

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuhakikisha Sekta ya Elimu inapata mwelekeo...

UKURASA WA 3

### BILIONI 149/- ZATENGWA BIMA YA AFYA KWA WOTE

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 149 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa bima ya afya kwa wote ambapo muswada wake unatarajiwa kupelekwa...

UKURASA WA 5

### WIZARA YAAGIZA MAGARI YALIYOKAMATWA YAACHIWE

WIZARA ya Kilimo imemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Philemon Sengati, kuyaachia magari...

## Hatima tozo miamala ya simu keshokutwa

UKURASA 2

MICHEZO MTIBWA YACHOMOA WA KIMATAIFA NAMUNGO FC UK.23
MAONI, KATUNI UK.6

# Hatima tozo miamala ya simu keshokutwa

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SERIKALI imesema hatima ya malalamiko ya wananchi kuhusu tozo ya miamala ya simu itajulikana keshokutwa baada ya kamati iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kumaliza na kukabidhi kazi yake kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji ya serikali katika mambo mbalimbali.

Akijibu swali kuhusu hatua iliyofikiwa na kamati iliyoundwa na Rais Samia katika utekelezaji, alisema majibu hayo yatatolewa keshokutwa na wananchi watajua nini hatima ya tozo hiyo ya miamala ya simu.

"Kamati iliundwa na Rais ikiongozwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, na Waziri Teknolojia ya Habari na Mawasilinao, Dk. Faustine Ndugulile, tayari imeshakamilisha tathimini yake na kazi hiyo kukabidhiwa kwa waziri mkuu na Agost 31, mwaka huu, itatoa maelekezo kuhusu tozo hiyo ya miamala ya simu," alisema Msigwa

Pia alisema wananchi wanapaswa kuwa wavumilivu kwa kuwa serikali yao iliweka tozo hiyo kwa lengo la kuharakisha baadhi ya majukumu.

"Tozo hii kama Waziri Mwigulu, anavyoiita kuwa ni tozo ya mshikamano, hivyo Watanzania hatuna budi kuipokea kwa kuwa itasaidia katika kuharakisha kukamilisha baadhi ya miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa barabara maeneo ya vijijini," alisema Msigwa

Pia alisema kwa kipindi kifupi tangu kuanza kwa tozo hiyo, serikali imepata Sh. bilioni 22 ambazo zimepelekwa katika tarafa ambazo hazijawahi kuwa na vituo vya afya toka uhuru.

Alisema katika maeneo hayo zimepelekwa takribani Sh. milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo vya afya katika tarafa husika.

"Kwa hiyo malalamiko ambayo hivi sasa wananchi wanalalamika sana kuhusu tozo hizi za miamala ya simu tayari kamati imeyafanyia kazi kwani hii tozo ipo kisheria. Tusingeweza kufanya kitu kwa sababu bunge ndilo lilipitisha sheria, hivyo kama tungefanya kinyume tungevunja sheria lakini tuwe wavumilivu hadi mwisho wa mwezi huu tutapata majibu ya uhakika kutoka serikalini," alisisitiza.

Kadhalika, alisema kuwa serikali inatambua kilio cha wananchi na haipo kwa ajili ya kumuumiza mtu.

"Watu wanahoji kuwa Rais amesema wananchi wameikubali tozo wakati wao hawakushirikishwa bila kujua kuwa wabunge ndio wawakilishi wao katika hili wao ndiyo walipitisha tozo hii ya miamala ya simu kwa niaba yao," alisema Msigwa.

Akizungumzia utaratibu wa mpya ukusanyaji kodi ya pango la ardhi kwa kutumia mfumo wa mita za Luku, Msigwa alisema utaratibu huo ndio umeanza lakini malalamiko yanayotolewa yataendelea kufanyiwa marekebisho.

Hata hivyo, alisema kuwa wamiliki wa nyumba ndio watakaohusika katika malipo ya kodi hiyo na si wapangaji kama ambao hivi sasa wameonekana kulalamika juu ya kodi hiyo.

# Kizimkazi kupaisha utalii wa Tanzania

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema amerejea nyumbani kwao Kizimkazi kwa ajili ya kukiletea maendeleo kijiji hicho na kuanika mikakati yake ya kupaisha utalii nchini.

Akifunga Tamasha la Kizimkazi jana kijijini huko anakotoka, Rais Samia alisema: "Nipo tayari kuwaletea maendeleo, hiki ni kijiji nilichozaliwa, baba yangu na mama yangu wamezikwa kijijini hapa, kuna msemo unasema 'mzarau kwao mtumwa'."

Rais alisema katika tamasha hilo ameambatana na wazungu wakiwa na kamera kwa ajili kupiga picha vivutio vya utalii kijijini huko na atazunguka nao Tanzania nzima ili kuitangaza nchi.

Alisema tamasha hilo litasaidia kutangaza fursa za kiuchumi ikiwamo shughuli za utalii, kijiji hicho kikiwa sehemu ya mkakati huo kikisifika kwa fukwe nzuri na samaki aina ya pomboo.

Rais Samia alisema serikali inatarajia kujenga bandari kubwa kijijini huko pamoja na hospitali ambayo itasaidia kutoa huduma na kuharakisha maendeleo.

Alisema serikali ina mpango kabambe kutangaza fursa zote za kiuchumi ikiwamo gesi asilia na uchumi wa bahari.

Mkuu wa Nchi alisema tamasha hilo lina malengo ya kuwaweka pamoja Wanakizimkazi na kudumisha umoja, kulinda na kudumisha mila na desturi zao ili zisitoweke.

Alisema lengo lingine ni kuhamasisha kujenga shughuli za maendeleo, akifungua nyumba za madaktari na shule.

Alisema vijiji havina zahanati na kituo cha afya, hivyo kutajengwa kituo kikubwa cha afya ili kuipunguzia mzigo wa wagonjwa Hospitali ya Mkoa (Makunduchi).

Rais Samia alisema kuna haja kuitangaza nchi ili kujiuza zaidi na mwakani nchi itafanya sensa ili kujua idadi ya wananchi na kujipanga vizuri katika mipango ya maendeleo. Aliwataka wananchi kushiriki katika sensa hiyo.

Pia aliwataka wananchi wote kuchukua tahadhari ya kutosha kujikinga na maradhi ya COVID-19 ambapo katika tamasha hilo wananchi wengi walijitokeza kuchanja.

"Niishukuru Benki ya CRDB kwa kulifadhili tamasha hili kwa kutujengea nyumba za madaktari, ninawashukuru NBC kwa gari la wagonjwa, pia NMB kwa mchango mkubwa walioutoa," alisifu.

Alisema amekubalina na ombi la kutunisha Mfuko wa Elimu ili kuboresha Sekta ya Elimu katika mkoa huo.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, alisema wanategemea kujenga soko la kisasa kijijini Kizimkazi na aliishukuru CRDB kwa kusimamia maendeleo ya mkoa huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema benki hiyo ni mshirika mkubwa wa maendeleo, hivyo itashirikiana na SMZ na SMT kuleta maendeleo kwa wananchi.

# 300,000 wachanja chanjo corona nchini

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SERIKALI imesema watu 300,000 mpaka sasa wameshapatiwa chanjo ya UVIKO-19 inayotolewa bure nchini.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utoaji wa chanajo ya UVIKO-19.

Alibainisha kuwa tangu kuanza kwa utoaji wa chanjo hiyo nchini, takriban watu 300,000 wamechanjwa na mwitikio umeonekana kuwa mzuri.

Msigwa alisema kuwa pamoja na mwitiko kuwa mzuri, hivi sasa serikali inapanga kuanzisha utaratibu wa kuwafuata wananchi katika maeneo yao hasa walioko vijijini na kuwapatia chanjo hiyo.

Msigwa alisema wananchi ambao bado hawajapata chanjo hiyo wanashauriwa kujitokeza kwa wingi ili kuchanjwa na kujiweka katika mazingira mazuri ya kuzilinda afya zao.

"Wataalamu wa masuala ya afya wanasema kuwa mtu aliyechanja, akipata ugonjwa wa corona yupo katika eneo zuri la kutibiwa na kupona kuliko yule ambaye hajachanja," alisema.

Msigwa alisema licha ya chanjo kutolewa, wananchi wanatakiwa kuendelea kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya ikiwamo uvaaji wa barakoa, kunawa mikono na kuepuka mikusanyiko isiyokuwa ya lazima.

"Ndugu wanahabari, tutoe elimu kwa wananchi ili waitumie vizuri hiyari yao na kwenda kuchanja lakini pia ninyi wanahabari ni kundi pia hatarishi, lazima mpate chanjo ili kujiondoa katika eneo hatari," alisisitiza.

Alisema lazima Watanzaia wasikilize wataalamu wa afya ili kupata maarifa sahihi ya kujikinga na ugonjwa wa corona badala ya kuendelea kusikiliza watu wasiokuwa na utaalamu.

"Kila mtu kweli anayo haki ya kuabudu na serikali haina dini, lakini serikali haitakuwa tayari kuona mtu anawapotosha wananchi wake kuhusu chanjo na kukaa kimyaa, hili haliwezi kutokea," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na malalamiko yaliyokuwapo ya gharama kubwa ya vipimo vya ugonjwa wa corona mipakani, serikali imeondoa gharama za upimaji wa kipimo cha haraka na cha PCR imepunguza gharama kutoka Dola za Marekani 100 hadi 50.

Msigwa pia alikanusha uvumi uliopo katika mitandao ya kijamii kuwa serikali imewarejesha kazini watumishi waliondolewa kwa kuwa na vyeti vya kughushi.




Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Kamishna wa Polisi mstaafu, Robert Boaz, akipunga mkono juu ya gari, wakati wa gwaride maalum la heshima lililoandaliwa kwa ajili ya kumuaga katika viwanja vya Chuo cha Taaluma ya Polisi Kurasini, mkoani Dar es Salaam jana, baada ya kumaliza utumishi wa umma kwa mujibu wa sheria. **PICHA: JESHI LA POLISI.**

HABARI KITAIFA

# Bilioni 149/- zatengwa bima ya afya kwa wote

Na Joseph Mwendapole, DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 149 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa bima ya afya kwa wote ambapo muswada wake unatarajiwa kupelekwa kwenye vikao vya Bunge vinavyoanza Jumanne wiki ijayo.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alibainisha hayo jana, jijini Dodoma alipofungua mkutano wa wahariri na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Alisema wanufaika wakuu wa kwanza wa mpango huo watakuwa Watanzania wa kawaida ambao hawana uwezo wa kukata bima ya afya.

Msigwa alisema ingawa muswada huo unatarajiwa kuwasilishwa kwenye mkutano wa Bunge, serikali iliona ni busara kutenga fedha mapema.

"Kutokana na umuhimu wake, serikali iliona ni heri kutenga kabisa fedha za kutekeleza mpango huo kabla hata muswada haujawasilishwa bungeni ili ukifikishwa na kupitishwa, fedha za utekelezaji ziwe tayari," alisema.

Aliipongeza NHIF kwa kuendelea kuboresha huduma zake na kupanua wigo wa utoaji wa huduma hizo ambapo kwa sasa makundi mbalimbali na watu binafsi yamekuwa yakijiunga na mfuko huo.

Msigwa alisema tangu kuanzishwa kwake miaka 20 iliyopita, mfuko huo umekuwa ukikua na kutanua huduma zake kwa kuwafikia Watanzania wengi zaidi ambao wananufaika na huduma zake.

"Mfuko huu ulianza kama mchicha mwaka 2001 lakini sasa umekuwa kama mbuyu. Ninawapongeza sana viongozi wa NHIF lakini wakati tukiupongeza mfuko, tuipongeze pia serikali ya awamu ya sita kwa dhamira yake ya dhati ya kuwekeza katika Sekta ya Afya," alisema.

Msigwa alisema serikali ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya na ndiyo sababu kwenye bajeti yake ya mwaka huu imetenga Sh. trilioni 1.4 kwa ajili ya sekta hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Benard Konga, alisema wakati wa kuanzishwa kwake mfuko huo ulipata vikwazo vikubwa vya upinzani kutoka kwa umma ambao wakati huo haukujua umuhimu wake.

Alisema pamoja na vikwazo hivyo, serikali haikukata tamaa kwa kuwa iliendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima ya afya na hatimaye wananchi wengi walikubaliana na kujiunga.

Alivishukuru vyombo vya habari kwa kuendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima ya afya kwa na kiwango kikubwa vimefanikiwa kuwashawishi wananchi kuona umuhimu huo.

Konga alisema NHIF sasa imekuwa ikitoa mikopo ya dawa na vifaa tiba kwa hospitali na vituo vya afya, lengo likiwa ni kuboresha huduma za afya kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Alisema miongoni mwa mafanikio ambayo NHIF inajivunia ni kujenga Hospitali ya Benjamin Mkapa mkoani Dodoma na kuipa vifaa vyote vya tiba.

Alisema NHIF imeiwezesha pia Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kutoa tiba ambazo awali watu walilazimika kwenda kuzipata nje ya nchi ikiwamo upandikizaji wa figo.

Vilevile, alisema mbali na MNH, mfuko pia umeiwezesha Taasisi ya Mifupa (MOI) vifaa tiba na dawa na kuiwezesha Hospitali ya KCMC iliyoko Mkoa wa Kilimanjaro kuzalisha mitungi ya gesi kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa COVID-19.

Alisema kwa sasa KCMC ina uwezo wa kuzalisha hadi mitungi ya 400 ya gesi ambayo husambazwa kwenye maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kusaidia kupambana na ugonjwa huo.

Alisema NHIF imefanikiwa kuingia mikataba na hospitali na vituo mbalimbali vya afya kwa ajili ya kutoa matibabu kwa wanachama wake na kwamba asilimia 60 ya mapato ya vituo hivyo yanatoka NHIF.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akizungumza na wanafunzi wa ufundi katika chuo cha ufundi stadi cha Lutherani Mafinga, mkoani Iringa juzi. Wanafunzi hao ni kati ya vijana 14000 wanaolipiwa gharama za masomo na Serikali kupitia programu ya ukuzaji ujuzi nchini. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Majaliwa ajivunia maboresho elimu

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema serikari inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuhakikisha Sekta ya Elimu inapata mwelekeo mpana na kutengeneza fursa kwa watoto wa Kitanzania kutimiza ndoto zao za kusoma katika ngazi zote mpaka vyuo vikuu.

Amesema katika kufanikisha hilo, serikali imeendelea kuboresha miundombinu kwa shule za msingi, sekondari na kuongeza idadi ya vyuo vikuu nchini, lengo likiwa ni kuwaandaa watoto kutimiza ndoto zao.

Waziri Mkuu alisema hayo jana alipokuwa katika mwendelezo wa ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo mkoani Tabora, akitembelea Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Tabora na Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Tabora ambako pia alifurahishwa na matokeo ya ufaulu wa shule hizo kimkoa na kitaifa sambamba na maboresho ya miundombinu yaliyofanywa katika shule hizo kongwe.

"Mheshimiwa Rais kaleta fedha nyingi sana za Sekta ya Elimu. Kaleta Sh. bilioni moja, akaleta tena Sh. milioni 500 na fedha nyingine Sh. bilioni saba ambazo ninaamini zimeshafika na zitajenga madarasa 590 ikiwa ni maandalizi ya kuwapokea watoto wa kidato cha kwanza.

"Hizi Sh. bilioni saba ni sehemu ya Sh. bilioni 29 ambazo zimesambazwa kwa ajili ya Sekta ya Afya na Elimu, makusanyo ambayo yametokana na miamala," alisema.

Waziri Mkuu alisema kuwa hivi karibuni Rais Samia alitoa kibali cha kuajiri walimu wa masomo ya sayansi ili kukabiliana na uhaba wa walimu katika masomo ya sayansi na kuweka uwiano sawa wa ufundishaji na ujifunzaji baina ya walimu na wanafunzi.

"Tumefurahi sana kuona kuna Watanzania wenzetu wanajitolea, tunajua wanafanya kazi, ninapenda kuwahakikishia kuwa serikali inalitazama suala hilo kwa umakini mkubwa na ninaiagiza TAMISEMI kuhakikisha walimu hawa wapewe kipaumbele katika ajira, wameonyesha uzalendo wa hali ya juu," aliagiza.

Akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Tabora, Majaliwa alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha shule zote kongwe zinakarabatiwa na kuzirudisha katika ubora ili kuwa na mazingira rafiki ya ujifunzaji na ufundishaji.

Hali kadhalika, Waziri Mkuu aliliagiza Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Tabora kuweka utaratibu na kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika shule hizo.

# Serikali yatoa tamko Denmark kufunga ubalozi wake nchini

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI ya Tanzania imesema imesikitishwa na hatua ya Serikali ya Denmark kuamua kufunga shughuli za ubalozi nchini ifikapo mwaka 2024.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amebainisha hayo masikitiko ya serikali kufuatia hatua hiyo ya Denmark.

Amesema masikitiko yao hayo yamezingatia jitihada kubwa zinazofanywa na serikali kufufua na kuimarisha diplomasia na uhusiano na nchi rafiki ikiwamo Denmark, kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini na kuimarisha demokrasia na utawala wa sheria.

Waziri huyo aliyasema hayo jijini Washington D.C, Marekani juzi wakati wa mazungumzo kwa njia ya mtandao na Flemming Moller Mortensen, Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo wa Denmark kufuatia ombi la waziri huyo kuzungumza na Waziri Mulamula.

Waziri Liberata alisema yuko Marekani kwa ziara ya kikazi na kwenye mazungumzo hayo, alimweleza Waziri Mortensen kwamba pamoja na hatua hiyo iliyochukuliwa na Denmark, ni matarajio ya Tanzania kuwa Serikali ya Denmark itaendelea kushirikiana na Tanzania kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuunga mkono ajenda za Tanzania katika Umoja wa Ulaya, Umoja wa Mataifa na majukwaa mengine ya kimataifa.

Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo wa Denmark, Mortensen, alisema uamuzi wa kufunga shughuli za ubalozi wo Tanzania ni wa kisiasa na haukuwa rahisi na kwamba umefikiwa kutokana na vipaumbele vipya vya Serikali ya Denmark kwenye ushirikiano wa maendeleo kama ilivyoainishwa kwenye mkakati wake mpya uitwao 'The World We Share'.

Kwa mujibu wa Waziri Mortensen, mkakati huo mpya unaitaka Denmark kufanya kazi kwa ukaribu zaidi na nchi zenye machafuko na migogoro hususan katika Ukanda wa Sahel, Pembe ya Afrika na nchi jirani na hizo ambazo zina matatizo ya kisiasa.

Kadhalika, waziri huyo alisema kutokana na Tanzania kufikia hatua nzuri ya maendeleo, Denmark imeamua sasa kufanya kazi kwa ukaribu na nchi tajwa ambazo alisema ndio zenye uhitaji zaidi na kwamba hatua hiyo haimaanishi uhusiano na urafiki kati ya Denmark na Tanzania unakufa au kufifia.

RIPOTI MAALUM

# Kilichojificha ndoa za babu na mjukuu

Na Waandishi Wetu

KILA siku watu wanaoana na neno ndoa linabaki palepale katika msamiati endelevu, wenza wa jinsia tofauti wenye umri unaoendana wanaingia kwenye ubia wa maisha kimila, imani na kisheria, kiunganishi kikuu hapo ni mapenzi.

Hata hivyo, wataalamu wa walezi na ubia huo wanaenda mbali kwamba mapenzi ni kipengele tu na kuna mazito katika tafsiri 'maisha'.

Hapo katika tafsiri kuu 'maisha' ndiyo leo hii kumeingia utata wa babu kumpata mwenza ambaye ni mjukuu, wenyewe wakiwabatiza jina la 'baby'.

Bibi pia hayuko nyuma na 'shallo balo', mhitimu wa sekondari miaka michache iliyoisha anasaka ajira akitokea kwa mama na baba.

Mara zote katika maisha hayo muoaji, mtoa uamuzi, mmiliki uchumi na pekee anayefaidi na mwoga kupindukia wa penzi hilo ni ama babu au bibi huyo.

Je, nini tatizo katika sosholojia hii ya ndoa? Mkazi wa Sinza wilayani Kinondoni mkoani Dar es Salaam, Amina Chibule, anasema uhusiano wa aina hiyo unachagizwa na kile anachokiita tamaa ya vijana kuishi maisha mazuri bila kujali madhara ya kiafya.

"Inasikitisha hawa mabinti wadogo sasa wanaongoza kuvunja ndoa za watu maana wanaparamia waume za watu na wazee huko mitaani.

"Yaani hawafikirii kabisa kwamba 'huyu baba kwa umri wake lazima atakuwa na familia' na pia wanaona kama fasheni kwa kuwa baba hao ndio wanawapa jeuri ya fedha. Kama mzazi, sifurahishwi kabisa na jambo hili," analalamika.

Hamis Shaaban (57), mkazi mwingine wa Sinza anashauri nchi iwe na sheria ya kudhibiti uhusiano wa aina hiyo baina ya watu wazima na vijana wenye umri mdogo.

"Kwa kweli hili suala ni la kusikitisha. Ninafikiri wengi wanaofanya haya mambo akili zao haziko sawa. Hivi unawezaje kujihusisha kimapenzi na binti mdogo ambaye kiumri ni sawa na mjukuu wako?

"Haiingii akilini kabisa. Ningeshauri serikali, ninafikiri kwa sasa hatuna sheria, tuweke sheria kali dhidi ya mzee yeyote atakayejihusisha kimapenzi na binti au kijana mdogo," anashauri.

Natalia Mpalanga (22), mkazi wa Riverside wilayani Ubungo mkoani Dar es Salaam, anasema anajisikia vibaya kuona vijana wenzake wanatenda kile anachokiita kukurupukia maisha wakiamini kuwa na uhusiano wa kimapenzi na watu wazima watakuwa na uhakika wa kutunzwa na kutimiziwa mahitaji yao yote.

"Vijana wengi wana tamaa ya vitu vizuri, mafanikio yanahitaji kuwa na subira, tunapaswa kuweka juhudi katika masomo na kujishughulisha na ujasiriamali," anasema.



Sheikh wa mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum. **PICHA: MTANDAO**

### USTAWI WA JAMII

Wataalamu wa masuala ya ustawi wa jamii wanasema ndoa za babu au bibi na mjukuu zinasababishwa na mambo mengi ikiwamo umasikini, tamaa, mikumbo na maumivu ya uhusiano wa kimapenzi uliopita.

Mhadhiri Msaidizi katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii mkoani Dar es Salaam, Catherine Banda, anainyoshea kidole kadhia hiyo, akifafanua:

"Mzee kuoa au kuwa na uhusiano wa kimapenzi na binti mwenye umri mdogo inaweza ikawa imesababishwa na baba mtu mzima kupoteza mwenza wake akiwa uzeeni.

"Katika mazingira hayo, hali ya upweke inamfanya atafute binti mdogo wa kuishi naye ili kumsaidia zile intimate needs (mahitaji ya ndani). Wengi wanahofu kuchukua watu wazima wenzao kwa kuwa wote wanakua hawana nguvu.

"Hii inamfanya mzee kwenda kutafuta binti mwenye umri mdogo, lakini msingi wa uhusiano wao unakuwa sio sahihi kabisa.

"Pia kuna tatizo la mabinti kuwa na uhusiano na mtu mzima ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi. Hii inatokana na imani kuwa watu wazima wana kipato kikubwa, hivyo kurahisisha maisha na binti huyo kutatua shida zake kwa haraka.

"Wapo mabinti ambao ni wanafunzi wa vyuo wanatoka kimapenzi na watu wazima ili wasaidiwe kifedha hata kama wanafunzi hao wanapata sapoti kubwa kutoka kwa familia zao, jambo hili sio jema

"Vijana wengi wanataka mambo makubwa ilhali hawana uwezo kifedha. Wanataka wawe na magari na simu za bei kubwa. Hizi tamaa zao ndizo zinawaponza hadi wanaingia kwenye uhusiano wa namna hii," Catherine anaonya.

Mtaalamu huyo wa ustawi wa jamii anabainisha kuwa vijana wa kiume wamekuwa wakitumbukia katika uhusiano wa kimapenzi na mama au bibi zao kutokana na uvivu wa kufanya kazi, hivyo wanakubali kwenda kulelewa.

"Kwa ujumla, suala hili sio sawa kwa ustawi wa jamii kwa sababu linakiuka taratibu za kiutamaduni. Mapendekezo yangu ni kwamba elimu ya uhusiano lazima itolewe kwa vijana ili wafanye uamuzi sahihi juu ya nani anastahili kuwa naye kwenye uhusiano wa kimapenzi," anashauri.

### VIONGOZI WA DINI

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi Inayoshughulika na Masuala ya Ndoa, Familia na Malezi Tanzania (TaMCare), Dk. Enock Mlyuka, anakosoa ndoa za babu na mjukuu, akisisitiza kuwa ndoa ni kitovu cha familia na malezi.

Dk. Mlyuka ambaye pia ni Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), anasema kinachochangia vijana kuingia kwenye uhusiano wa kimapenzi na watu wazima au binti kuolewa na mtu mwenye umri mkubwa, ni makuzi ya vijana hao wanayotoka nayo kwenye familia zao.

"Hawa wameanza kuharibiwa kuanzia kwenye familia zao, mambo wanayofanya wameona wanakotoka, hawakuwekewa misingi bora ya kujitambua, nidhamu na maadili. Wakifikia utu uzima wanaingia kwenye uhusiano wakiwa hawajitambui sawasawa," anahadharisha.

Anataja jambo lingine ni anachokiita ulimbukeni binafsi, akifafanua kuwa kijana akikosa ajira, anakuwa na visingizio vya hali ngumu ya maisha na kuona heri alelewe na mtu mzima.

"Kitendo hicho kinamwondolea umakini wa kufanya uamuzi sahihi, anachokiangalia ni kutatua tatizo lililopo mbele yake, analelewa bila kujua mwanaume unapooa halafu ushindwe kutimiza majukumu yako, thamani inashuka, wengi wamejikuta badala ya kutatua tatizo, yanaongezeka mengine," anaonya.

Anataja sababu ya tatu ni kukosa maarifa, hivyo kijana kuingia katika taasisi ya ndoa bila kuielewa madai, misingi, kanuni na miiko yake.

"Wapo walioingia kishabiki wakidhani ndoa ni fedha wakati huo sio msingi wake. Tatizo lingine kubwa ni vijana kutokuwa na uhusiano mzuri na Mungu. Wana elimu ya utandawazi ambao unawaendesha katika ndoa zao.

"Haipiti siku sijapata simu au mtu amekuja ana mgogoro na mwenza wake. Nyingi unakuta mwanamke ni mkubwa kuliko kijana au wamepishana kidogo umri au umri unaofanana na nyingine unakuta wote ni watu wazima," anabainisha.

Nipashe Jumapili inatua mezani kwa Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, ambaye ana ufafanuzi kwamba sio kosa kijana kuoa mtu mzima au kuolewa na mtu aliyemzidi umri, lakini shida iko kwenye utu uzima wenyewe.

"Kuna utu uzima sana na utoto sana, kiutu na heshima haipendezi. Japokuwa dini haikatazi, lakini kuna vitu vya murua na heshima. Wakioana umri unaofanana au umri uliopishana kidogo, kunakuwa na heshima," anashauri.

Kiongozi huyo wa kiroho anasema vijana wa kike na kiume wanakimbilia kulelewa, wakiamini watu wazima wana fedha, hivyo kuwa na uhakika wa kuhudumiwa.

Anaonya kuwa ndoa nyingi za aina hiyo huwa hazidumu kwa sababu vijana hao baadae hukutana na wenye umri unaoendana nao na kusababisha migogoro.

* *Imeandaliwa na Haika Christopher (SJMC), Leyla Joho (TUDARCo) na Sechellah Nakamba (SJMC). Taarifa za ziada: Romana Mallya.*

# Serikali yaingilia shule iliyokataa wagonjwa

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

OFISI ya Udhibiti Ubora wa Elimu Kanda ya Kati imeuagiza uongozi wa Shule ya Wasichana Huruma jijini Dodoma kufuta barua yake iliyoelekeza haitapokea mwanafunzi yeyote kujiunga na masomo akiwa na tatizo la kiafya.

Barua hiyo iliyotolewa na shule hiyo yenye Kumbukumbu Na. HGS/DOM/7/2021, inaelekeza kuwa shule haitampokea mtoto mwenye tatizo la msio (allergy), vidonda vya tumbo, tatizo la moyo, kifafa na asthma.

Nipashe ilimtafuta Mdhibiti Mkuu wa Ubora wa Elimu Kanda ya Kati, Sospeter Magina, ambaye alibainisha kushangazwa na uamuzi wa shule hiyo.

"Unayo barua hiyo ya shule husika? Basi nipatie, ninakuomba hili niachie, nitakwenda huko kuonana na uongozi ili kubaini sababu za wao kufanya hivyo," alisema Magina.

Baada ya kuitembelea shule hiyo na kufanya ukaguzi, Magina aliiambia Nipashe kuwa uongozi wa shule hiyo umekiri kuwapo kwa barua hiyo.

"Wamesema kuwa ilikuwa ni tafsiri potofu tu kwani wao hawakuwa na nia mbaya ya kuwatenga watoto wengine, hata sasa wanao wanafunzi wenye matatizo hayo.

"Ambacho wanadai wao walitaka tu wazazi wasiwapeleke mbali na familia zao watoto wao na kutumia gharama kubwa kuwahudumia," alisema Magina.

Alibainisha kuwa kutokana na majibu hayo, ameuagiza ungozi wa shule hiyo kuifuta barua hiyo na kuacha kuitumia tena kama sehemu ya maelekezo kwa wazazi ambao watoto wao wanataka kujiunga na shule hiyo.

"Nimewaambia waifute barua hiyo na wameahidi kuifuta na kutoitumia tena," alisisitiza Magina.

Awali Nipashe pia ilifika ofisini kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, kufuatilia suala hilo, lakini alielekeza watafutwe wadhibiti wa ubora wa elimu na maofisa wengine wa ngazi za chini ili kulitafutia ufumbuzi.

"Siwezi kukujibu swali hilo kwa sababu sifahamu lolote, waulize wenyewe shule kwa nini wanafanya hivyo na kwa miongozo gani au waulize maofisa elimu wa mkoa au wilaya.

"Mimi Katibu Mkuu ni ngazi ya juu sana kwa jambo hilo kulisemea," alielekeza Dk. Akwilapo.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli, alisema amemwagiza mkurugenzi wake alifanyie kazi.

# Wizara yaagiza magari yaliyokamatwa yaachiwe

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WIZARA ya Kilimo imemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Philemon Sengati, kuyaachia magari zaidi ya 30 ya wafanyabiashara yaliyokamatwa yakiwa yamebeba mazao jamii ya kunde, wakamataji wakishinikiza kuwa yako kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani.

Naibu Waziri, Hussein Bashe, alitoa gizo hilo juzi jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kuzuiwa kwa magari hayo licha ya mazao hayo kwenye eneo hilo kutokuwa kwenye mpango wa uuzaji mazao kwa njia ya stakabadhi ghalani.

Alisema pamoja na Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, kumwandikia barua Mkuu wa Mkoa huyo kumtaka kuyaachia mazao na magari aliyokuwa ameyazuia, bado aliendelea kukaidi maelekezo hayo na kuendelea kuyashikilia.

"Agosti 10, mwaka huu, nilipata malalamiko kwa njia ya ujumbe mfupi wa maandishi kutoka kwa wafanyabiashara wa mazao wa mikoa ya Mwanza na Mara wakilalamikia kukamatwa kwa magari yao katika Mkoa wa Shinyanga na kulazimishwa kufuata utaratibu wa kuuza mazao hayo kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

"Baada ya kupokea malalamiko hayo nikamwandikia ujumbe mfupi kwa njia ya simu Mkuu wa Mkoa Shinyanga, Sengati, nikimtaka awaachie na kuwaruhusu kuendelea na utaratibu wao.

"Alikaidi ndipo Agosti 20, mwaka huu nilimwandikia barua nikimweleza kuwa katika mikoa ya Shinyanga na baadhi ya mikoa mingine hakuna mfumo wa stakabadhi ghalani lakini aliendelea kukaidi. Agosti 26, mwaka huu nikamwandikia barua nyingine akaendelea kukaidi," alisema.

Naibu waziri huyo alisema kutokana na hali hiyo, Wizara ilichukua uamuzi wa kuiandikia barua mikoa yote ambayo haitumii mfumo wa uuzaji wa mazao kwa njia ya stakabadhi ghalani ikiwataka kutowakamata wafanyabiashara wa mazao ya jamii ya mikunde ikiwamo choroko, mbaazi na dengu.

"Uamuzi wetu wa wizara kuandika barua kwa wakuu wa mikoa ni kutokana na ukaidi uliofanywa na Mkuu wa Mkoa huyo wa Shinyanga, hivyo sasa wizara tunatoa tamko la kutaka magari yote yaliyozuiwa Mkoa wa Shinyanga maeneo ya Tinde na mazao ambao yameshushwa kwenye magari kuachiwa huru ili wafanyabiashara waendelee na utaratibu wao walioamua kuutumia kuuza mazao yao," alisisitiza.

Alisema mwenye mamlaka ya kubadilisha utaratibu wa uuzwaji wa mazao uliopangwa ni Waziri wa Kilimo na si vinginevyo, hivyo kitendo kilichofanywa na uongozi wa mkoa huo ni kukiuka utaratibu na kufanya uonevu na usumbufu kwa wafanyabiashara hao.

Bashe alisema vitendo hivyo vya kibabe katika utekelezaji wa majukumu ndivyo vimekuwa vikidumaza Wizara ya Kilimo na kusisitiza kuwa hawatakuwa tayari kuvivumilia.

"Hatuwezi kukalia vitu hivi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais halafu tukavumilia vitendo vya kionevu kama hivi vinavyofanywa dhidi ya wafanyabiashara wa Kitanzania.


## NOTISI / TANGAZO

**DESTENI COMPANY LIMITED, MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, ,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART, MOPEH COMPANY LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| NA | JINA LA MDAIWA | TAWI ALILOKOPA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SAIDI AKILIMALI KALILWA | UBUNGO | SAIDI AKILIMALI KALILWA | NYUMBA | MWASONGA-KIGAMBONI | 13/9/2021 NA KUENDELEA |
| 2 | KOKUBELWA PAUL NG'AMBEKI | AGGREY | ANTHON AARON ICHWEKELEZA | GARI T 988 DNN TOYOTA CALDINA | TABATA CHAMA - ILALA | 14/09/2021 NA KUENDELEA |
| 3 | BETTY BENSON KAGARUKI | TEMEKE | BETTY BENSON KAGARUKI | NYUMBA | MSAKUZI – WILAYA YA UBUNGO | 17/9/2021 NA KUENDELEA |
| 4 | KASSIM MBARUKU KASSIM | MBAGALA | ZAHORO SAID ZAHORO | NYUMBA | MBANDE-KISEWE | 14/09/2021 NA KUENDELEA |
| 5 | MADALE KIDS PALACE | TEGETA | CRUCIAL INVESTMENT LIMITED | NYUMBA YA BIASHARA | MADALE | 15//9/2021 NA KUENDELEA |
| 6 | ESTHER JOHN GICHOGO | KARIAKOO | FATUMA HASSANI MGWAMI | NYUMBA | KITUNDA-MACHIMBO | 16/09/2021 NA KUENDELEA |
| 7 | SALOME JOSEPH LIGANGA | TEGETA | SALOME JOSEPH LIGANGA | NYUMBA | BUNJU 'B' | 14/09/2021 NA KUENDELEA |
| 8 | AITA WOINDUMI NATHAN | TEGETA | AITA WOINDUMI NATHAN | NYUMBA | WAZO | 17/09/2021 NA KUENDELEA |
| 9 | SHABANI SELEMANI KIGODI | TEGETA | SHABANI SELEMANI KIGODI | NYUMBA | NYAKASANGWE | 16/09/2021 NA KUENDELEA |
| 10 | SIAJALI ELIDADI KAVUYE | TEGETA | SIAJALI ELIDADI KAVUYE | NYUMBA | MUUNGANO-GOBA | 20/09/2021 NA KUENDELEA |
| 11 | HABIBU OMARY NYAKASENE | TEGETA | HABIBU OMARY NYAKASENE | NYUMBA | WAZO-KISANGA | 21/09/2021 NA KUENDELEA |
| 12 | OMARY JUMA RASHIDI | TEGETA | OMARY JUMA RASHIDI | NYUMBA | WAZO-KISANGA | 23/09/2021 NA KUENDELEA |
| 13 | HENRY MTINDA MATATA | MWANZA | HENRY MTINDA MATATA | NYUMBA INA HATI | PLOT NO. 1579 KITALU "A" LUCHELELE NYEGEZI MWANZA | 15/09/2021 NA KUENDELEA |
| 14 | MTONDI SIAGI KICHELE | MWANZA | MTONDI SIAGI KICHELE | 1.BOMA LINA HATI 2.NYUMBA INA HATI | 1.KIWANJA NAMBA.1467 KITALU "B" NYAMALANGO MWANZA 2.KIWANJA NAMBA 202 KITALU "HH" NYAKATO ILEMELA MWANZA | 14/09/2021 NA KUENDELEA |
| 15 | FELISTER BILLIAM MACHA | MWANZA | JOAN RAPHAEL JAPHET | NYUMBA INA HATI | KIWANJA NAMBA 91 KITALU "C" KISHILI MWANZA | 16/09/2021 NA KUENDELEA |
| 16 | MICHAEL WAMBURA MNEMA | MWANZA | MICHAEL WAMBURA MNEMA | NYUMBA | IPO KASHISHI MWANZA | 17/09/2021 NA KUENDELEA |
| 17 | RICHARD RAPHAEL KATARAMA | MWANZA | BARNABAS FELIX | NYUMBA | IPO KABUHORO KIRUMBA MWANZA | 20/09/2021 NA KUENDELEA |
| 18 | DICKSON ANICETH GREEN | MWANZA | DICKSON ANICETH GREEN | NYUMBA | KIWANJA NAMBA 4056 KITALU "B" BUJINGWA ILEMELA MWANZA | 21/09/2021 NA KUENDELEA |
| 19 | ROBERT THOMAS SERERYA | MWANZA | ADELA PETER EZEKIEL | 1.KIWANJA 2.NYUMBA 3.KIWANJA CHENYE MSINGI | 1.HATI MILIKI NAMBA 59276 KITALU "D" KISHILI NYAMAGANA MWANZA 2.HATI YA MAUZIANO – KANGAYE "A" NYAKATO ILEMELA MWANZA 3.HATI YA MAUZIANO NSUMBA ILEMELA MWANZA | 22/09/2021 NA KUENDELEA |
| 20 | MICHAEL OCHIENG OTANG | MWANZA | MICHAEL OCHIENG OTANG | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO – NUNDU MECCO ILEMELA MWANZA | 23/09/2021 NA KUENDELEA |
| 21 | MARY JOHN DEUS | TANDALE | MARY JOHN DEUS | NYUMBA | KIMARA | 14/09/2021 NA KUENDELEA |
| 22 | DAVID ANDREA LEKASI | UBUNGO | DAVID ANDREA LEKASI | NYUMBA | KIBAHA | 14/09/2021 NA KUENDELEA |
| 23 | SHANI WAPALILA | ARUSHA | SHANI WAPALILA | NYUMBA | MOSHONO | 15/09/2021 NA KUENDELEA |
| 24 | MILLANS KISOKA | ARUSHA | MODEST MICHAEL KISOKA | NYUMBA | MOROMBO | 16/09/2021 NA KUENDELEA |
| 25 | FATUMA JUMA | ARUSHA | FATUMA JUMA | NYUMBA | NJIRO | 20/09/2021 NA KUENDELEA |
| 26 | REHEMA HAMIS JEMEDARI | TANDALE | REGINA NJENI MWAKASAGULE | NYUMBA | MSASANI | 14/09/2021 NA KUENDELEA |
| 27 | MUNA SAID NGALENI | UBUNGO | MUNA SAID NASSORO NGALENI | NYUMBA | KIGOGO | 15/09/2021 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuziatalazimikakulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0765999000/ 071439933/0689349477/ 0713604044/ 0674821287/ 0785335544/ 0785242219**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

216429702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maagizo ya Rais kwa Jeshi la Polisi yafanyiwe kazi ipasavyo

**WIKI** hii Rais Samia Suluhu Hassan alifungua kikao kazi cha maofisa wa Jeshi la Polisi na kutoa maagizo mbalimbali ambayo kwa kiasi kikubwa yamekuwa kikwazo cha utendaji ndani ya taasisi hiyo yenye dhamana ya kulinda usalama wa raia na mali zao.

Rais Samia pia alilitaka jeshi hilo kukaa na wadau kuangalia uwezekano wa kurekebisha sheria ya kuweka mtu mahabusu, jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa kwa miaka mingi. Hiyo ni kutokana na baadhi ya watuhumiwa kukaa muda mrefu mahabusi bila kufikishwa mahakamani. Kwa kawaida, sheria inataka mtu akae mahabusu ndani ya saa 48 kabla ya kufikishwa mahakamani au vinginevyo.

Sababu hasa kubwa ya watu kukaa mahabusu jela muda mrefu, mbali na ile ya polisi ni hoja ambayo imekuwa ikitolewa na jeshi hilo ya kutokukamilika kwa upelelezi.

Katika hotuba yake, Rais hakuuma maneno hasa aliposema hadi Agosti 22, mwaka huu, idadi ya mahabusi katika magereza mbalimbali nchini ilikuwa inakaribiana na wafungwa. Kwa mujibu wa Rais hadi tarehe hiyo kulikuwa na mahabusi 15,194 wakati wafungwa ni 16,542.

Baadhi ya mahabusi hao ni waliokaa vipindi tofauti kuanzia wiki, mwaka mmoja hadi mitano. Kutokana na idadi hiyo, Rais alitoa wito kwa jeshi hilo kwa kesi ambazo wanaona upelelezi hautakamilika, watuhumiwa watolewe ili wakafaidi uhuru wao wakiwa nje.

Licha ya kutaka waachiwe kwa sababu hiyo, alitaka Jeshi la Polisi kujifunza kutoka kwa nchi zingine ambazo mtuhumiwa hukamatwa baada ya kukamilika kwa upelelezi, hivyo baada ya kukamatwa anapelekwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Mambo mengine aliyoyasema Rais ni baadhi ya askari polisi kutuhumiwa kutokutenda haki kwa jamii, akitolea mfano wa tukio la baadhi yao kudaiwa kupora nyama jijini Dar es Salaam; matumizi makubwa ya nguvu; na watuhumiwa kufia mikononi mwa polisi kutokana na kuburuzwa, kupigwa virungu na hata vipigo vikali.


Mambo hayo ambayo Rais aliyazungumzia, pamoja na rushwa, yamekuwa yakizungumzwa mara kwa mara kuwa yanalitia doa Jeshi la Polisi katika utendaji kazi wake wa kila siku.

Ni wazi kwamba si aksari na maofisa wote wanaojihusisha na vitendo hivyo na hatimaye kulichafua jeshi zima lakini kama wahenga wasemavyo samaki mmoja akioza wote wameoza, ndivyo inavyoonekana katika jamii.

Kwa mantiki hiyo, maagizo hayo ya Rais iwe changamoto kwa Jeshi la Polisi kujitathmini na kurejea katika mstari wake kwa kutenda haki ikiwamo kutekeleza kauli yao ya 'Usalama wa Raia'.

Ni imani kwamba kwa kuwa Rais ni Amirijeshi, maagizo yake ni amri, hivyo uongozi wa Jeshi la Polisi, chini ya mkuu wake, Inspekta Jenerali (IGP), Simon Sirro, utatekeleza na kuchukua hatua madhubuti katika kuhakikisha nidhamu ndani ya jeshi inarejea na kila mmoja kuwajibika katika nafasi yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Benki zaidi zishirikishwe urasimishaji wa makazi

**URASIMISHAJI** wa makazi ya watu unazidi kupata nguvu kutokana na baadhi ya wadau kujitokeza kushirikiana na serikali kwa ajili ya kufanikisha kazi hiyo ili kusaidia wananchi kunufaika na ardhi yao.

Miongoni mwa wadau hao ni Benki ya NMB ambayo hivi karibuni ilizindua huduma mpya ya mkopo wenye riba nafuu, ili kuwasaidia wananchi wa kipato cha chini kutekeleza takwa la kisheria la kurasimisha makazi yao.

Huduma hiyo iliyopewa jina la 'NMB Plot Loan' inaendeshwa kwenye Programu ya Kitaifa ya Urasimishaji wa Makazi ikitekelezwa kwa ushirikiano kati ya benki hiyo na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Benki ya NMB inalenga kuwasaidia wananchi kulipia gharama zote za urasimishaji wa makazi kuanzia upimaji wa viwanja hadi uandaaji wa hatimiliki, huku mhusika akilipa kidogo kidogo ndani ya miaka miwili.

Kwa ujumla ni kwamba, hatua hiyo ni zuri na ni fursa kwa wananchi kuichangamkia, ili kurasimisha makazi yao, kwa ajili ya faida yao ya baadaye, kwa kuzingatia kwamba, kwa ardhi ni mali hasa inapokuwa imepimwa.

Lakini pamoja na hayo, ili kuharakisha kazi ya kurasimisha makazi ya watu, ninadhani kuna haja ya kushirikisha benki nyingi zaidi zotoe mchango wa kufanikisha kile ambacho kinakusudiwa na serikali.

Ni kweli kwamba moja ya mambo ambayo serikali inakazania na kuyawekea msukumo, ni kuhimiza wananchi kurasimishaji makazi yao, kwa lengo la kuwanufaisha pale wanapokuwa wanamiliki kitu ambacho kimepimwa.

Si vibaya serikali ikaingia mkataba na benki zote ili zipite mitaani waliko wamiliki wa makazi, ili kutoa mikopo kuliko kuacha hata watu wa umri mkubwa kwenda kujipanga foleni benki kwa ajili mkopo.

Ninaamini kwamba suala hilo likishirikishwa benki nyingi, itakuwa ni rahisi kufikiwa wananchi wengi kwa haraka, hivyo nionavyo, ni serikali kuangalia uwezekano wa kuingia mkataba na wadau hao wengine.

Hatua hiyo itasaidia kurasimisha makazi mengi zaidi kwa muda mfupi, lakini pia wale ambao watakuwa wamefikiwa, watatumia ardhi yao kukopa fedha benki na kufanya shughuli nyingine za maendeleo.

Kimsingi, urasimishaji wa makazi una faida nyingi ikiwamo kupanda kwa thamani yake, ardhi kutumika kama dhamana mahakamani, lakini pia mtu kuwa na amani na uhakika wa ardhi yake.

Hayo yote mtu anakuwa na uhakika nayo kutokana na kwamba eneo ambalo yupo, limeruhusiwa kisheria, hivyo mhusika anaweza kufanya shughuli zake za maendeleo bila hofu kwamba huenda akapokonywa ardhi yake.

Ili kuwafikia watu wengi zaidi, njia ambayo inaweza kusaidia, ni kushirikisha wadau wengine, hasa serikali kuingia mkataba na benki nyingine zaidi kama ilivyofanya kwa NMB, kusaidiana katika kazi ya urasimishaji wa makazi.

Ninatambua kuwa, ardhi, iwe kiwanja au nyumba, thamani yake hupanda pale inapokuwa imepimwa na kupima ardhi ni kurasimisha makazi, na faida nyingi hupatikana baada ya ardhi kurasimishwa.

Wakati mwingine, huenda baadhi ya watu wanashindwa kurasimisha makazi yao kwa kukosa fedha za kulipia gharama za urasmishaji, NBM inaweza kuwa imeleta unafuu, lakini ninadhani kuna haja kushirikisha benki nyingine zaidi.

Pamoja na hayo, yawezekana wapo baadhi ya watu ambao hawajui umuhimu wa urasimishaji wa makazi. Hao nao ni vyema wakapewa elimu kuhusu umuhimu wa urasimishaji huo, ili wajue faida zake.

Wakishazijua, inakuwa ni rahisi wao kujitokeza kwa wingi kurasimisha makazi yao kwa ajili ya manufaa yao ya baadaye, kwa kuwa tayari watakuwa na dhamana ya uhakika wanayoweza kuitumia.

Ikumbukwe kuwa, mtu akirasimisha makazi yake, anapatiwa hatimiliki, hivyo kumfanya awe na sifa za kukopesheka katika benki yoyote na kupata fedha za kumwezesha kufanya shughuli za maendeleo.

Lakini pamoja na hayo, ingependeza zaidi kama serikali itaingia mkataba na benki nyingine zaidi kwa ajili ya kuharakisha kazi ya urasimishaji wa makazi ili Watanzania wapate hatimiliki

## SAFU

### KWA MASLAHI YA TAIFA



**Pascal Mayalla**

# Kuupata uhiari wa chanjo, tusitishane bali kunahitajika uhamasishaji tu

NI Jumapili nyingine tena, tunapokutana kwenye safu hii Kwa Maslahi ya Taifa.

Leo naendelea na hoja kuhusu chanjo ya corona kwa Watanzania, nikiendelea kuwa chanjo hiyo ni hiari.

Kutokana na hali hiyo, sisi wahamasishaji tuendelee kuhamasisha kwa uhuru na wapinga chanjo nao waachwe wapinge kwa uhuru.

Lakini kutokana na umuhimu wa chanjo kwa taifa na ili kuwahamasisha Watanzania wengi wajitokeze kwa hiari yao, kunahitajika uelimisha umma wa nguvu, ambao utazijibu hoja zote za wapinga chanjo, kwa majibu ya kitaalamu.

Lakini tufanye nini ili kufanikisha hilo? Ninapendekeza, mosi, kwa vile chanjo ni hiari, tusitumie vitisho vya polisi kwa wapinga chanjo. Tutumie elimu kuwaelimisha, waelewe, wakubali chanjo kwa hiari yao na wale wanaopinga kwa sababu wanapinga tu au kwa hoja zisizo na mashiko, wasioelimishika wapuuzwe.

Pili, nivipongeze vyombo vyote vya habari kwa kazi nzuri ya uhabarishaji umma na utoaji wa elimu ya jinsi ya kujikinga na Corona. Pamoja na pongezi hizo, vinatakiwa kutoa elimu ya chanjo kwa kuandaa vipindi maalum vya redio, televisheni, makala za uelimishaji umma magazetini na kwenye mitandao ya jamii.

Tatu, kwenye kitu kinachoitwa kitaalam, "reaching out strategies", Tanzania kama taifa, hatuna muongozo wowote rasmi kuhusu utoaji elimu ya chanjo. Hakuna kipindi chochote maalumu cha umma kuhusu elimu ya kinga dhidi ya corona kwa umma.

Matangazo yapo na mahojiano pia yapo lakini tangazo ni tangazo, mahojiano ni mahojiano. Kunatakiwa vipindi maalum vya utoaji elimu ya kujikinga na corona pamoja na chanjo yake.

Kwenye vyombo rasmi vya habari, bado kuna kazi kubwa ya kufanya katika utoaji elimu. Vyombo vya habari vinavyotoa elimu ya kinga na elimu ya chanjo, bado vinafanya kwa kujitolea na si kama wajibu (obligation).

Kwenye janga kama hili, jukumu la utoaji wa elimu kwa umma, hasa elimu ya kinga na elimu ya chanjo, lisiachwe kwa vyombo vya habari pekee kuendelea kujitolea tu, bali jambo hili liwe jukumu la wizara yenye dhamana ya afya na zile ambazo zimehusika moja kwa moja na masuala ya jamii.

Taasisi hizo za serikali hususan wizara, kwa kuwa suala hilo ni mtambuka na linahitaji jitihada za pamoja katika kuvishinda vita hivyo (corona), kwa kushirikiana na wadau ziandae mkakati maalum wa mawasiliano (specific communication strategy) ya elimu kuhusu ugonjwa wenyewe na chanjo.

Mkakati huo uhusishe, pamoja na mambo mengine, utengenezaji vipindi maalum vya elimu kwa umma kwa kuwatumia wataalamu wa afya kuzungumzia mambo ya kitaalamu huku viongozi na watu mashuhuri wenye ufuasi mkubwa wakitumika kuchanja na kuhamasisha watu wachanje. Vipindi hivyo visambazwe kwenye vyombo vyote vya utangazaji, magazeti na TV mtandao ili virushwe katika muda ambao watu watakuwa wanasikiliza au kutazama kwa wingi (prime time).

Makala elimishi kuhusu chanjo ya corona, ziandaliwe na kusambazwa kwenye magazeti yote. Kwa vile corona haina kinga wala tiba, msaada pekee kwa sasa ni chanjo, hivyo Watanzania waelimishwe kuhusu chanjo na hoja za wapinga chanjo zijibiwe kitaalamu.

Tatu, Watanzania kwa sasa tuko milioni 60, hivyo wanaopaswa kuchanja ili taifa liwe salama ni angalau milioni 30. Ili kuliokoa taifa letu, na kuifanya chanjo ikubalike kwa wote, lazima tufanye uelimishaji umma, ikiwamo kuandaa matamasha ya chanjo, kwa kuwatumia wasanii maarufu kina Daimond Platnum, Hamonaize na Ali Kiba, kufanya matamasha ya bure, maeneo ya wazi kama Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Nne, wasanii watunge nyimbo za kuelimisha umma kuchanja na kuwe na matangazo kupitia magari ya buurudani (road shows) huku wacheza shoo wakitoa burudani kwenye magari hayo.

Tano, pamoja na media kuendelea kujitolea, ili vifanye jambo la maana, lazima viwezeshwe, hivyo matajiri wa Tanzania, mashirika, kampuni na taasisi mbalimbali zihamasishwe kuchangia ili kusaidia vyombo vya habari kutimiza hili kwa kudhamini vipindi vya uelimishaji umma kuhusu chanjo ya corona.

Sita, wahenga wanasema kilio huanza na mfiwa. Kutokana na ukweli huo, binafsi na kampuni yangu ya PPR, tayari nimejitolea ninafanya kazi ya uelimishaji umma na uhamasishaji kupitia makala zangu za 'Kwa Maslahi ya Taifa'. Pia kila nikiliakwa kipindi cha Jicho Letu Ndani ya Habari, kinachorushwa na Star TV kila Jumamosi asubuhi, lazima nihamasishe chanjo.

Hivi karibuni kipindi cha TV cha "Kwa Maslahi ya Taifa, kitarushwa hewani kupitia vituo sita vya TV nchini. Nimeshazungumza na wakuu wa TV kubwa nchini wamekubali kuwa kipindi hicho kirushwe katika vyombo vyao.

**Pascal Mayalla**
**Media Consultant**
**Mob. +255 754 270403**
**pascomayalla@gmail.com**

### FMADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



**Na Joseph Kulangwa**

# CCM ilivyong'ata na ing'ate sasa

UKITAKA kujua uimara wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) huna budi kuwakumbuka Mwalimu Julius Nyerere, Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete, John Magufuli na sasa Samia Suluhu Hassan.

Lakini pia Pius Msekwa, Daudi Mwakawago, Rashidi Mfaume Kawawa, Horace Kolimba, Lawrence Gama, Yusuph Makamba, Wilson Mukama, Abdulrahman Kinana, Bashiru Ally na sasa Daniel Chongolo. Hao ni wenyeviti na makatibu wakuu mtawalia wa chama hicho.

Kundi la kwanza lote ni la marais wa tangu Tanganyika na hatimaye Tanzania. Wanaheshimika na wanaenziwa kwa kuwa na mchango mkubwa wakulifikisha Taifa hili hapa lilipo.

CCM inajivunia kuwa chama ambacho kwa kipindi chote imetoa marais tofauti na vyama vingine, lakini hiyo haimaanishi kwamba vyama vingine vya upinzani haviwezi kuzaa marais wakaja kuiongoza nchi hii kama hao waliotangulia.

Walioiongoza CCM wakapita, kila mmoja aliacha alama yake na ndiyo sababu CCM ikaendelea kuwa na nguvu na kujikita kwenye madaraka tangu kuzaliwa kwake hadi sasa, ikipitia milima na mabonde, ikitumia hekima na mabavu kuongoza.

Hata hivyo, imesababisha nchi kuwa amani na utulivu licha ya malalamiko ya hapa na pale, hususan kutoka kwa mahasimu wake wa kisiasa, vyama vya upinzani, kwamba imekuwa ikiwadhulumu kwa kutumia Dola. Bashiru alipata kutoa ushuhuda huo.

CCM imekuwa siku zote na taratibu zake za kushughulikia mambo yake ya ndani na nje, hususan kuhusu wanachama na viongozi wake, hasa pale utokeapo mtafaruku. Mwanachama au kiongozi anapoacha njia na kufuata yake. Anapokosa nidhamu.

Kuwajibishwa ndani ya chama hicho pale ulipokiuka taratibu si ajabu, walitimuliwa na wengine kusimamishwa. Uongozi haukuangalia we nani wala una nafasi gani ndani ya chama hicho.

Rais wa Awamu ya Pili Zanzibar, Alhaji Aboud Jumbe, katika miaka ya themanini, alipochafua hali ya hewa Zanzibar, aliondoshwa.

Wako wengi tu waliokumbana na rungu la CCM, wa hivi karibuni ni wale wa mwaka 2015 wakati wa kinyang'anyiro cha urais, akitafutwa mgombea wa chama hicho pale Dodoma, kukatokea mtafaruku miongoni mwa wanachama vigogo.

Walioibuka na kupinga uamuzi wa CCM kuteua watu fulani ndani ya Halmashauri Kuu, vigogo watatu; Emmanuel Nchimbi, Sophia Simba na Omar Kimbisa, waliposimama na kumkatalia Mwenyekiti Kikwete, kuwa aliingia na majina yake mfukoni.

Watatu hawa tena usiku mkubwa, wakatoka nje ya kikao na kuzungumza na wanahabari kupinga hatua hiyo, wakitaka 'mtu wao' naye awamo kwenye kinyang'anyiro. CCM haikuangalia we ni nani, ikawaweka pembeni sawia.

Baada ya uchaguzi na mshindi kuibuka, Dk. Magufuli kuwa Rais wa nchi, na akaapishwa na kuanza cheche, mara zikasikika sauti kwenye simu, zikimsimanga. Huku na kule, waliothibitika kuhusika wakabanwa.

Naikumbuka sana CCM ya Kinana, Nape na Chongolo. CCM iliyozunguka nchi nzima kuzungumza na wananchi, kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi. CCM iliyotamka bayana kwamba kuna mawaziri mzigo, ikijua kabisa kuwa mawaziri hao ni uzao wake, lakini kwa nini imumunye maneno?

Ni kweli, ilikuwa CCM imara isiyotaka mchezo ndani na nje yake, ili mradi ilihakikisha wananchi wanaishi maisha ya bila kuonewa wala kunyonywa, kwa kuwa serikali iliyotakiwa kuhakikisha wananchi wanaishi maisha mazuri, ni ya uzao wake.

Kwa mapenzi ya Mola, mwaka huu Machi tukaondokewa na Mwenyekiti wetu wa CCM, Rais Magufuli na nafasi yake akaishika Rais Samia, akaja na kaulimbiu yake ya 'Kazi Iendelee!' Kwa kuwa Bashiru alishaondoka CCM wakati huo, chama kikaona bora sasa mikoba apewe Chongolo.

Chongolo alikuwa na Kinana, hivyo anajua nini walikifanya enzi hizo za mawaziri mizigo.

Akaingia wakati huu ambao tuna Uviko-19. Huku siasa huku ugonjwa. Rais wetu akapambana mpaka tukapata chanjo ya Jenssen kutoka Marekani, ikatuona masikini sisi na kutusaidia angalau dozi milioni na ushei za kuanzia.

Tulipochanja wakaibuka wanachama wa CCM kutoa msimamo ambao tulitarajia ni wao na familia zao, lakini bahati mbaya wanaambukiza wengine, hivyo kuacha kujitokeza. Wanampinga Mwenyekiti, Rais, hivi CCM ile haiwezi kujirudia sasa?

***Alamsiki!***

## KONA YA UKWELI

# Tuviachie vyombo vya usalama vichunguze tukio la mauaji Dar



Na Thobias Mwanakatwe

AGOSTI 25, 2021 itabaki katika kumbukumbu kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam na nchi kwa ujumla kutokana na tukio la mauaji ya watu watano, wakiwamo askari watatu wa Jeshi la Polisi.

Tukio hilo ambalo lilitokea katika eneo la daraja la Selandar jirani na zilipo ofisi za Ubalozi wa Ufaransa, lilizua taharuki kubwa kwa wananchi waliokuwa jirani na eneo hilo wakiwamo waliokuwa kwenye magari ambao walilazimika kukimbia kujaribu kuokoa maisha yao.

Baada ya tukio hilo ambalo Kamishna wa Operesheni wa Jeshi la Polisi, Liberatus Sabas, alitoa taarifa kuwa watu wanne wamefariki dunia na sita kujeruhiwa kwenye mapambano ya kurushiana risasi yaliyotokea makutano ya barabara za Kenyatta na Kinondoni jirani na Ubalozi wa Ufaransa.

Akasema kati ya watu wanne walifariki dunia watatu ni askari polisi, huku mmoja akiwa mtumishi wa kampuni ya ulinzi ya SGA.

Kilichonisukuma kujikita katika hoja hii ni namna ambavyo kumekuwa na maneno mengi na uzushi mwingi kwenye mitandao ya kijamii.

Kwanza nianze kwa kutoa pole sana kwa Jeshi la Polisi kwa kuondokewa na askari wake ambao kimsingi walikuwa wakitekeleza majukumu yao ya kulinda usalama wa raia na mali zao ambalo ndilo jukumu muhimu la jeshi hilo.

Tukio hilo limeacha simanzi kubwa na taharuki kwa sababu limekuja pasipo kutarajia na siku ambayo makamanda wa polisi wa mikoa na maofisa wengine wa jeshi hilo walikuwa Dar es Salaam kwenye mkutano wa uzinduzi wa mwongozo wa utendaji kazi wa jeshi hilo. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi.

Kinachonishangaza, kumekuwa na hisia na hukumu nyingi kuhusiana na tukio la hilo lililopoteza maisha ya watu watano.

Ugaidi, kisasi, chuki vimetajwa kama sababu na baadhi ya watu ili mradi kila mmoja amesema anavyodhani ni sawa kwenye mitandao ya kijamii ambayo kimsingi asilimia kubwa wanaitumia vibaya kupotosha mambo mengi si katika tukio hili tu.

Aidha, wapo waliohoji kwa nini polisi walichukua uamuzi wa kumuua mtuhumiwa badala ya kumpiga risasi hata miguuni ili wamhoji na kupata ushahidi kama kuna watu anashirikiana nao kwenye uhalifu.

Najiuliza unamkamataje mtu mwenye bunduki nzito, anayerushiana risasi na polisi na ambaye ameshaua askari wanne na yuko tayari kuua hata zaidi? Kama angejisalimisha kwa kuweka bunduki chini na kunyoosha mikono au kulala kifudifudi na bado akauawa hapo sawa.

Njia pekee ya kuokoa uhai wa angalau mtu mmoja zaidi asiye na hatia ilikuwa kumuua. Hapo hakuna kosa upande wa polisi. Hakuna 'conspiracy' yoyote. Kwa ujumla. tukio hilo ni baya, linaloleta picha mbaya ndani na nje ya nchi. Ni tukio ambalo tukiruhusu kila mmoja atoe hukumu yake, azungumze apendavyo balaa lake liko mbeleni maana watu wataikataa hata ripoti ya kipelelezi ambayo Rais Samia Suluhu Hassan ameagiza itolewe haraka.

Wakati palishakuwa na hali ya utulivu Dar es Salaam baada ya mabadiliko yaliyofanywa katika Jeshi la Polisi, jambo hili lisipofuatiliwa kwa kina na kwa umakini litaleta doa. Je ni kweli polisi walitaka kumdhulumu dhahabu zake? Je, ni suala la ugaidi? Je, ni tatizo la kiakili? Je, ni suala kisiasa? Yote tuyasubirie yatolewe na vyombo vya usalama vinavyochunguza tukio hilo.

Kilichoanza kunishtua na kunishangaza na pengine ikawa si mimi pekee yangu ni kuanza kuhusisha jambo hili na mambo siasa. Naona huu ni ushamba kuanza kuhusisha tukio hili mapema hata kabla uchunguzi haujakamilika, maana hakuna chama kinachoweza kuhimiza mauaji ya watu wake. Kama mtu ni mwovu ashughulikiwe yeye binafsi na si taasisi, dini au kabila lake.

Nina imani kubwa na Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kwamba wenye jukumu la kuitoa ripoti ya tukio hilo wataisimamia kweli kwa faida ya nchi. Kama ni ugaidi hatua stahiki za kuufuatilia mtandao huo zitachukuliwa na kama kuna huo uchafu wa dhuluma nao usemwe maana kuna wasio waaminifu.

Nadhani tuviachie vyombo vya ulinzi na usalama vichunguze kwa kina tukio hilo lakini mambo ya kuendelea kulumbana na kueneza taarifa kwenye mitandao ambazo hazijawa na uhakika si jambo zuri.

Ndiyo maana hii mitandao ya kijamii katika baadhi ya nchi imedhibitiwa ni kutokana na mambo kama haya watu wanakosa uzalendo na nchi yao.

Nirudie kulipongeza Jeshi la Polisi lilivyokabiliana na tukio hilo lakini pia niupongeze ushujaa binafsi wa askari walioonekana katika 'video clips' walivyokabiliana na muuaji.

Wakati uchunguzi ukiendelea familia ya muuaji isielemezewe uovu wakati wa kutafuta kiini cha jambo hili. Wabaki kuwa wasaidizi muhimu kwa dola na si watuhumiwa muhimu.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

***Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com***

## DARASA LA NDOA

# MATUMIZI YA SIMU YANAVYOATHIRI UHUSIANO BAINA YA WANANDOA- 3



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0655865555

Mawasiliano katika ndoa ni daraja linalounganisha ndoa na ni injini inayofanya ndoa iwe katika mwendo. Pale mume na mke wanapokosa mawasiliano mazuri baina yao, huondoa uhai katika uhusiano.

Mapenzi yanakauka kama shamba la mpunga. Hivyo ni muhimu sana wanandoa kufanya tathmini ya mawasiliano yao katika ndoa ili kuimarisha ndoa zao huku kila mmoja akizingatia kuwa, kumjua mume au mke kunaanzia na mawasiliano. Mahali popote palipo na mawasiliano mazuri pana mafanikio makubwa. Mahali popote pasipo na mawasiliano lazima matatizo yatatokea.

Wanandoa wajifunze kuratibu mawasiliano yao vizuri ili yasiwe kero na kusababisha kuharibu uhusiano wao kwani hakuna mtu anayependa kupuuzwa au kuonekana kwamba yeye si muhimu.

Epuka kuzama katika simu au kufanya mawasiliano mengi ya simu wakati ukiwa na mwezi wako. Huo ni muda wake na wewe. Ni haki yake ya msingi ya kuwa pamoja na wewe. Anahitaji ukaribu wako, anahitaji umakini wako, anahitaji kusikilizwa, na anahitaji joto lako. Unatakiwa kumsikiliza mwenzi wako na kuwa karibu naye kimwili na kihisia kwani anakuhitaji wewe zaidi kuliko kitu kingine.

Mwenzi wako ni mtu muhimu zaidi kuliko hao unaowasiliana nao mara kwa mara katika simu. Kumbuka, kule kuwa na muda na simu yako zaidi kuliko mwenzi wako, ndiko kunakoweza kuleta shaka na tatizo. Jali zaidi uhusiano wako na mumeo au mkeo kuliko simu yako ili kutunza utulivu (harmony) katika ndoa.

Ikiwa wanandoa hawapeani muda wao kwa wao, hupoteza hisia za mapenzi juu yao na nafasi kubwa sana ya kufahamiana vizuri. Simu za mkononi zitumike kwa mujibu wa uhitaji na kwa nidhamu. Kila jambo ni muhimu kufanyika kwa kiasi na utaratibu. Ni muhimu kutunza heshima ya ndoa na uhusiano.

Simu za mkononi ni kama kisu. Kisu kikitumika vizuri kitaleta manufaa lakini kikitumika vibaya, huweza kusababisha madhara. Mawasiliano kwa njia ya simu za mkononi ni muhimu sana. Hata hivyo, simu hizi zinaweza kuleta amani au mfarakano miongoni mwa wanandoa kutegemea na jinsi zinavyotumika.

Yafaa simu zitumike vizuri kwa nidhamu ili kutunza heshima ya ndoa na wanandoa wenyewe. Mwanandoa mwenye nidhamu katika matumizi ya simu (mobile phone etiquette) atajua mahali na wakati unaofaa au usiofaa wa kutumia simu yake.

Uhuru katika kushika au kutumia simu ya mwenzi ni jambo jema na linalofanywa na baadhi ya wanandoa wanaoaminiana na kuheshimiana. Hata hivyo, inafaa kila jambo lifanyike kwa makubaliano na utayari wa pande zote mbili na siyo kwa amri au mashinikizo. Ni busara sana mke au mume kuwa na mtazamo chanya juu ya matumizi ya simu ya mwenzi wake.

Kwa msingi huu, wanandoa wanashauriwa kuacha tabia ya kupenda kushughulika na kufuatilia taarifa zilizomo katika simu za wenzi wao. Hivi ndivyo wanandoa wanaojitambua wanavyopaswa kuishi na kuendesha maisha yao.

Kama nilivyosema awali, simu ya mkononi ni chombo binafsi cha mawasiliano, hivyo wanandoa wanahitaji kuwa wastaarabu katika matumizi ya chombo hiki. Ni busara mke au mume kutokufanya jambo ambalo mwenzi wake hapendi ili kutunza amani na utulivu katika ndoa. Mke au mume kumbuka, yoyote unayotaka kutendewa, wewe uwe wa kwanza kumtendea mwenzi wako, kwani kumbadilisha mtu, huanza pale wewe unapoanza kubadilika kwanza ili kumfanya abadilike.

Wanandoa wajifunze kutenda yale waliyokubaliana na yanayowapa amani zaidi na siyo kuishi kwa kuviziana. Simu za mkononi zitumike kwa uzuri (decently) na kwa utaratibu (orderly manner). Simu za mkononi zikitumika vizuri kwa nidhamu, zitachangia katika kuimarisha ndoa na kuwafanya wanandoa kuwa na uhusiano wenye ladha (exciting).

- ***Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.***

AGOSTI 29, 2021
Nipashe

# MAISHA

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


## Faida za karoti ni hizi....



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Kuwa mbunifu kupangilia nyumba ya nafasi ndogo




## KATUNIKA

Ukurasa 16




# USO WENYE MAFUTA

## Njia hizi zitakusaidia kujing'arisha

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| S | A | N | I | F | U |
| A | | | | I | |
| I | N | A | | K | |
| | U | | T | A | I |
| | K | | | | P |
| K | A | T | I | Z | O |

## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## WATOTO

# PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
BIA, ZUA, PINDUA, MAISHA, ABIRIA, HUKUMU

## CHEKA



Alichokifanya Adaktari

MTOTO John alikuwa akilia baada ya kupigwa na wenzake wakati walipokuwa wakicheza mpira. Kaka yake alikuja haraka ili kujua nini kimemsibu.

Kaka: John unalia nini?

John: Kasim amenipiga baada ya kumwambia anipe mpira wangu

Kaka: Basi nyamaza twende nyumbani

John: Hapana mama akijua nimelia ataniadhibu

Kaka: Kwa nini?

John: Mama aliniambia shujaa huwa halii

Kaka: Hapana huo ni msemo tu, maana yake ni kuwa mvumilivu.

**SWALI**

Zao la Korosho linapatikana katika mikoa gani ya Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mauzauza ardhi ya mganga wa kienyeji kudhibiti wageni

KARIBU msomaji tuendelee na mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Utakumbuka wiki iliyopita tulijadili ardhi inavyoweza kukuinua au kukuangusha kimaisha. Nikatoa siri kwamba wenyeji katika eneo lolote la ardhi, mara nyingi wamekuwa kikwazo kwa wageni iwe ni kwa kuishi, kufanya kazi au kwa kilimo.

Nikasema wenyeji ni wale watu waliotangulia kuwepo mahali fulani kabla yako. Wengi wa wenyeji huwa ni watu wabaya kuliko unavyofikiria. Watu wengi hatma zao zimeamuliwa na wenyeji wa nchi (eneo). Na wengi hugundua hilo baadaye sana wakiwa tayari wameshajeruhiwa kimaisha.

Mpenzi msomaji, kabla sijakutajia mbinu wanazotumia wenyeji kukudhoofisha, hebu sikiliza ushuhuda wangu mwenyewe. Ni mashambulizi baada ya kununua kipande cha ardhi eneo la Mlandizi.

Ilikuwa mwaka 2011 niliponunua eneo lenye ukubwa wa ekari saba. Nilikamilisha taratibu katika ngazi zote kuanzia serikali ya kijiji hadi upimaji wa ardhi. Nikalishafisha na kuotesha mazao mchanganyiko ikiwemo miti ya miembe, mihogo, na viazi vitamu. Kilimo hiki nilianza mwaka 2013.

Hata hivyo, kilimo hiki kilikuwa na maruweruwe mengi kwani mimea ilionekana kustawi lakini kwenye mavuno ndio ilikuwa kitendawili. Mihogo na viazi vilikuwa vinaoza. Wenyeji walivuna vizuri lakini mimi hakuna kitu. Hata miembe ilipukutisha maua embe zikawa chache sana.

Nikajaribu kufanya upelelezi kuhusu wenyeji wa eneo lile. Nikahojiana na baadhi yao wakanimegea siri. Mwenyeji mmoja akaniambia kwamba yule mzee aliyeniuzia shamba ni mganga wa kienyeji. Akasema watu wengi pale walikuwa wananishangaa kujitosa kununua ardhi ile.

Akasema kabla yangu, eneo hilo lilishanunuliwa na wateja wawili na wote, pamoja na kutoa kiasi cha fedha za utangulizi, hawakuwahi kurejea tena. Na kwamba mzee wa shamba hilo alikuwa amelizindika na kwamba huwa ana nyoka humvisha shanga na kumuweka chini ya mti ulioko pale shambani.

Ndipo nikagundua kuwa ardhi ile tayari ilifungwa ili hata atakayenunua asifanikiwe. Kwa kuwa mimi namtumaini Mungu na siyo mwanadamu, nikaomba nguvu ya Mungu initetee kwa kuwa nilinunua eneo lile kwa haki na hakuna mgogoro. Nikaamini kwamba Mungu hujibu maombi kwa wakati wake. Nikapiga hatua kwa ujasiri bila kuogopa vitisho nikajenga nyumba ndogo pale shambani. Ilipofikia kwenye lenta vita ikaibuka wazi wazi. Mlinzi wangu akaanza kutishiwa na vilio vya bundi wawili ambao walikuwa wakija usiku na kutua juu ya jengo linalojengwa. Bundi hao walipokezana na paka aliyekuwa akilia usiku na kuparura mlango.

Nilipomwendea balozi wa kitongoji kumuuliza kunani, akanijibu kuwa hata yeye anapata vituko hivyo na kwamba hao ni washirikina. Akatoa siri kwamba pale kijijini kipo kikosi cha wachawi ambao wanasumbua sana. Akanitajia majina yapatayo nane.

Nilifanya maombi kusambaratisha kikosi hicho na ndani ya mwezi mmoja tishio pale shambani likakoma hadi leo. Hakuna mtu anayesogelea pale. Miaka miwili iliyopita nimeanza kuvuna mihogo na hata embe kati ya 500 na 600, jambo ambalo halijawahi kutokea. Mwaka huu embe zimebeba sana naamini Mungu atanipa mavuno mazuri.

Mpenzi msomaji, utaona jinsi wenyeji walivyo wabaya. Aliyeniuzia ardhi tayari alishainajisi kwa ushirikina wake. Yawezekana alishaitamkia ile ardhi kuwa kila atakayeinunua, hatakaa ni lazima aondoke.

Kadhalika wenyeji baada ya mimi kununua eneo hilo walitahayari. Kwanza kwa kuwa ni mwanamke wakihoji nawezaje kununua eneo kubwa vile. Pia walijua kuwa nitalibadilisha kutoka pori kuwa makazi.

Nilisema wiki iliyopita kwamba wenyeji siku zote humuona mgeni kuwa ni tishio kwao. Siku zote wenyeji hawataki wazidiwe na mgeni kwa chochote, iwe ni kimaendeleo au kimuonekano. Hivi sasa shambani ni shwari na nimetoa ekari moja kwa serikali ya mtaa kujenga zahanati na kituo kidogo cha polisi.

Mpenzi msomaji, nimetoa mfano huo ili upate kujua kwamba ardhi tunayokalia ina vita kubwa na wengi hawafahamu. Waweza kupanga nyumba kumbe imezindikwa. Unaota ndoto za ajabu ajabu, kumbe mwenye nyumba mchawi.

**Wiki ijayo nitamalizia mada hii kwa kutaja mbinu wanazotumia wenyeji dhidi ya wageni na jinsi ya kuwashinda. Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Tahadhari ya corona bado sana kwenye vyombo vya usafiri

MARA kadhaa viongozi wa serikali wametoa maelekezo kuhusu kujikinga na corona, ikiwa ni pamoja na namna ya kukaa ndani ya vyombo vya usafiri, uvaaji barakoa na kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka.

Ilifikia mahali kuwa usipovaa barakoa hutaruhusiwa kutumia chombo cha usafiri, lakini kwa sasa hali ni kawaida kama vile corona haipo. Hii inaonyesha kuwa bado wananchi hawajaona umuhimu wa kuchukua tahadhari.

Mathalani, katika kituo cha mabasi cha Magufuli, eneo la Mbezi Mwisho, wasafiri na wasindikizaji wanaingia na kutoka kituoni humo lakini bado hakuna tahadhari kubwa inayochukuliwa kwa kuwa hakuna utaratibu wa kulazimisha watu kuvaa barakoa.

Unapoingia kituoni humo unachoulizwa ni kama umeshalipa tiketi ya kuingia basi, lakini asilimia kubwa ya waliomo humo hawajavaa barakoa na hakuna vyombo vya kunawia mikono.

Watu wanaendelea na maisha utadhani corona haipo! Hata nje ya mabasi hakuna vitakasa mikono wala abiria haulizwi kuhusu barakoa bali wanaingia na ni kawaida kukuta wengi hawajavaa barakoa.

Hakuna ubishi kuwa corona ni tishio kwa sasa na watu wengi wameugua na wengine kupoteza maisha na husambaa zaidi kwenye vyombo vya usafiri ambako kuna mikusanyiko.

Maagizo ya viongozi mbalimbali kuwa ni lazima abiria au watu wanapokuwa kwenye mikusanyiko wavae barakoa yameishia hewani kwa kuwa hayana utekelezaji, jambo ambalo si sawa kwa kuwa ilipaswa kuwa na ufuatiliaji kuhakikisha kuwa watu wanajikinga na corona.

Nchi ambazo zimeruhusu mikusanyiko kwa sasa ni zile ambazo watu wake wameshachanjwa kwa maana ya kwamba nchi nzima wamechanjwa na wanahakikisha wanapokuwa kwenye mikusanyiko wanavaa barakoa, watakasa mikono. Yote hiyo ni kujikinga kwa kuwa hata mtu akichanja bado ana uwezekano wa kupata ugonjwa huo.

Kwa nchi bado watu hawajachanja inavyotakiwa wachache wameamua kusikiliza ushauri wa wataalam na kuchanja ila wengi wamebaki na msimamo wa kutochanja kwa sababu zao wenyewe.

Wataalam wamethibitisha kuwa mtu aliyechanja anakuwa ameongeza askari wa kumlinda mwilini na inapotokea mashambulizi yoyote, askari wale hupambana na kuwa washindi. Mtu huyo hata akipata corona, haitamyumbisha au kugharimu maisha yake kama yule ambaye hajachanja.

Ni muhimu nguvu ikaelekezwa kuelimisha wananchi kuchanja kama ambavyo inafanyika kwa baadhi ya nyumba za ibada ambazo viongozi wake wameamua kuwa mfano kwa kuchanja hadharani na wengine wakitoa maelekezo wa viongozi wengine wa kanisa hilo kufanya hivyo.

Ikifikia mahali Watanzania wote wenye umri wa kuchanja wakachanjwa ndipo tutaweza kuwa salama kwa kuwa tutapambana na kirusi kwa urahisi zaidi. Lakini hali ikiendelea hivi na watu hawachukui tahadhari zote muhimu kuna hatari ya kuendelea kupoteza watu wengi zaidi.

Wako ambao bado hawaamini kwamba corona ipo na inaua au watu wanaugua na kupata madhara ya muda mrefu kwenye mwili, lakini pia kuna gharama kubwa ya matibabu ambayo wakati mwingine familia zinashindwa kumudu.

Inashangaza mtu anakwenda hospitalini hajavaa barakoa na mara nyingi ni kwenye hospitali binafsi ambazo ni vigumu kulazimisha uvaaji wa barakoa. Hakuna ubishi hospitalini kuna mengi ikiwamo corona, hivyo lazima watu wajikinge lakini wako ambao wanakwenda bila tahadhari yoyote jambo ambalo si sawa kabisa.

Ifike mahali kwamba huingii kokote bila kuvaa barakoa, kutakasa mikono kwa sanitizer au kunawa kwa maji tiririka na sabuni, vinginevyo itachukua muda mrefu ugonjwa huu kupungua nguvu.


Kwa sasa ugonjwa umesambaa hadi vijijini na watu wanapoteza maisha, mbaya zaidi watu wanakwenda kwenye misiba na kukusanyika kama kawaida yaani wanaendeleza utamaduni wa kuomboleza kwa mikusanyiko kama kawaida, jambo ambalo halitakiwa.

Ni muhimu viongozi wa dini wa maeneo hayo kuhamaisha watu kuhakikisha wanavaa barakoa na kubadili taratibu za kuwafariji wafiwa, kwa kuwa unakuta mtu anajulikana kafa kwa corona lakini bado watu wataambatana kwa wingi na kumkumbatia au kumshika mfiwa, hata kama yeye hana anaweza kuambukizwa.

Ni muhimu kuchukua tahadhari, corona ipo na ineshakatisha maisha ya wengi na wengine wako hospitalini wanatetea uhai wao.

Pia viongozi wafuatilie utekelezaji wa maagizo yao, je, watu wanayafuata au waliongea na kuishia hewani? Na kama ndivyo basi kuwe na uwajibikaji ili kuokoa nguvu kazi na kupunguza uwezekano wa hospitali kuelemewa na wagonjwa.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**


Dida
JUST MARRIED

# MITINDO

Na Christina Mwakangale



## VAZI LA MAMA SAMIA

## Linavyofundisha vijana namna ya kuvaa

RAIS wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, zimekuwa gumzo ndani na nje ya nchi kutokana na upekee wa mitindo yake.

Hata anaposafiri kwenda nchi mbalimbali, watu wanakuwa makini kuangalia nguo gani anayovaa katika kutembelea shughuli mbalimbali na mwenyeji wake.

Hata hivyo, baadhi ya watu wanaita aina hizo za nguo kama 'Samia Style' kutokana na jinsi zinavyompa mwonekano mzuri na wenye heshima.

Kwa kawaida, vazi hilo linalotengenezwa kwa kitambaa kizito kiasi, hujumuisha koti refu lililokuwa na vifungo na uwazi katikati, siruali pana na kunogesha kwa hijab na viatu vifupi.

Katika kuweka nakshi zaidi, 'Samia Style' unaweza kubeba begi dogo la mkononi, huku ukiweka sawa na mawani ya rangi yoyote ile ili mradi yawe ya kiheshima.

Vazi hili lipo la kiheshima zaidi ni muhimu mvaaji atambue kwamba linafaa katika shughuli mbalimbali za kitaifa, mikutano, matembezi ya kifamilia, makongamano na kusafiria.

UREMBO

Na Mary Geofrey



# USO WENYE MAFUTA

## Njia hizi zitakusaidia kujing'arisha

WATU wengi hawapendi kuwa na mafuta usoni na ndio maana huhangaika kutafuta njia mbadala wa kuyaondoa ikiwamo vipodozi vyenye kemikali.

Ingawa kuna faida ya kuwa na uso wenye mafuta kwa kuwa kuupati mikunjo haraka kama uso mkavu, lakini wengi hawapendi kutokana na karaha ya kutokwa na jasho kila mara.

Kama unataka kuzuia hali hiyo, unaweza kufuata njia zifuatazo za kutunza uso wenye mafuta

Uso wenye mafuta lazima kuoshwa na 'facewash' sio sabuni za kawaida. Kuna facewash za kupunguza mafuta usoni. Madukani zinapatikana kwa wingi.

Uso wenye mafuta unaoshwa mara mbili au tatu kwa siku. Na pia ukirudi kutoka safari yako unaosha uso kwa maji ya baridi na 'facewash'.

Hutakiwi kutumia maji ya moto kuosha uso wenye mafuta kwa sababu yanazidisha joto na kuleta chunusi nyingi usoni.

Uso wenye mafuta na wenye chunusi nyingi hautakiwi kufanyiwa 'scrub', ukifanya hivyo chunusi upasuka na kutoa maji maji yanayosambaa na kuzalisha chunusi nyingi.

Mtu mwenye uso wa mafuta anatakiwa kusugua uso na shingo kwa barafu baada ya hapo unapaka vipodozi.

Unaweza pia kupunguza mafuta usoni kwa kusugulia ndimu usoni. Ndimu ina acid na hukata mafuta, kata ndimu kipande na sugua usoni.

Kaa nayo mpaka ikauke kisha nawa na maji ya bomba au ukipenda maji ya baridi ya fridge.

Mwenye mafuta mengi usoni hatakiwi kupaka lotion au mafuta kwa sababu inababisha chunusi kuongezeka.

Ikiwa una mtoko, siku moja kabla shinda na maji ya ndimu usoni na kabla ya kuanza kupaka vipodozi sugua barafu ya kawaida au ya maji ya ndimu na nawa kwa maji ya bomba au ya baridi kutoka katika fridge kisha paka vipodozi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Faida za karoti ni hizi....

KAROTI ni moja ya chakula kitamu, lakini kina umuhimu mkubwa katika kuboresha mwili wa binadamu.

Chakula hiki ni sawa na daraja muhimu katika kuimarisha mwili kutokana na kuwa na utajiri wa vitamin na madini.

Na hizi ni baadhi ya faida zitokanazo na ulaji wa karoti

Karoti husaidia kuimarisha macho kuona vizuri hasa wakati wa usiku, pia inasaidia kuondoa matatizo ya mzio (aleji) kwenye macho mfano macho kuwasha sababu ya vumbi.

Hurutubisha seli mwili na kuzifanya zisizeeke haraka. Hii inatokana na uwapo wa Vitamin A ambayo ni muhimu katika kuimarisha uwezo wa macho kuona.

Karoti huifanya ngozi iwe nzuri na yenye afya, kama utatumia kurutubisha ngozi yako kwa kupaka kwenye ngozi.

Karoti husaidia kuondoa sumu na taka mwilini, inaondoa mafuta yasiyotakiwa katika ini na kuliwezesha lifanye kazi vizuri, kusafisha njia ya haja kubwa na kusaidia kupata choo vizuri.

Karoti zinasaidia kufanya fizi na meno kuwa imara na kuchochea uzalishwaji wa mate.

Pia inasaidia kuzuia kiharusi, baadhi ya watafiti kutoka vyuo vikuu duniani wanasema ulaji wa karoti sita kwa wiki husaidia kutopata kiharusi.

Madaktari hao wamegundua pia karoti zinatibu tatizo la kupoteza kumbukumbu kwa wazee.

Karoti husaidia kuongeza kinga mwilini kwa sababu tabia asilia ya karoti kuwa na antibakteria ambao husaidia kuzuia kinga za mwili.

Karoti pia ina Vitamin C muhimu kwa kusisimua seli nyeupe za damu ambazo ni sehemu muhimu katika kinga ya mwili.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Kuwa mbunifu kupangilia nyumba ya nafasi ndogo

ASILIMIA kubwa ya wakazi mijini wanaishi katika nyumba za kupanga.

Kutokana na hali halisi ya maisha, ni familia za kiafrika chache zenye uwezo wa kumudu kupanga nyumba kubwa ya kutosheleza familia nzima.

Kama ilivyo desturi kwa familia hizo, nyingi hujumuisha zile zinazojulikana kwa lugha ya kigeni 'extended family', hivyo familia kuwa kubwa pasipo kulingana na kipato kilichopo cha kumudu kupanga nyumba kubwa.

Kwa hiyo ili umudu kuishi katika sehemu ndogo ya nyumba kulingana na uwezo uliopo na ukubwa wa familia, lazima ubunifu na akili nyingi itumike katika kupangilia vitu ili nafasi katika nyumba hiyo itosheleze mahitaji.

Pia kuna haja ya kupunguza baadhi ya vitu visivyo vya lazima.

Kwa upande wa uwekaji wa samani katika nyumba hiyo ndogo ni lazima uhakikishe kwamba zile zenye umbo dogo na ambazo zitakuwa na sehemu ya kuhifadhia vitu vingine au zenye matumizi zaidi ya moja.

Kwa mfano meza ya televisheni, unaweza kuweka zenye kuhifadhia vitu vingine hususani vitabu na vinginevyo.

Pia, tumia sehemu ya ukuta 'kudizaini' kwa ajili ya kuweka vitu vingine ikiwamo vyombo hasa jikoni.

Na ili ufanikishe kwa vitu vichache unavyokuwa umepanga kuweka kwenye nyumba hiyo ndogo, ni vizuri kupima kwanza ukubwa wa eneo lako kabla ya kutengeneza samani zako.

Epuka kuweka vitu ovyo bila kufanya tathmini ya uhakika, na ikiwezekana orodhesha idadi ya vitu na aina inavyotakiwa kuingia kwenye nyumba hiyona ambavyo havichukui nafasi kubwa.

Tumia ubunifu katika sehemu za kona za nyumba yako kuweka fenicha zako, hususani meza na televisheni na uhakikishe nazo zinakuwa ni zile ambazo hazichukui nafasi kubwa.

Jambo kubwa la kuzingatia katika suala la kupangilia vitu katika nyumba yako ndogo ni ubunifu na kuepuka vitu ambavyo havina ulazima.

Usiweke kitu ilimradi umeona kwa jirani yako ameweka, isipokuwa kwa kuzingatia umuhimu wake na nafasi uliyonayo kwenye nyumba yako.

Pia katika siku za hivi karibuni kwa upande wa samani za ndani, zipo hata ambazo unaweza kuzikunja, na kama ukifanikiwa kupata za namna hiyo inakuwa bora zaidi katika kuhifadhi nafasi.

Kwamba unazitumia pale unapoona inahitajika tu, na unaweza kuamua kuzikunjua mchana halafu usiku ukakunja.



## Namna ya kuchagua meza ya mbao ya Televisheni



JE, unataka kuweka runinga yako kwenye meza ya mbao, lakini hujui namna ya kuipata? Basi usipate shida, hizi ni baadhi ya dondoo muhimu za kuchagua meza nzuri ya kuwekea runinga yako.

1: Angalia muundo wa meza kama utaendana na mpangilio wa vitu vyako kwenye sebule kama vile sofa, meza ya kahawa na rangi ya ukuta.


2: Hakikisha meza yako ina vitu muhimu kama sehemu ya kuwekea deki, king'amuzi na vitu vingine muhimu.


3: Chagua aina nzuri ya mbao, usichukue mbao laini ambazo kutokana na mitindo ya maisha unayoishi inaweza kuharibika haraka na kukupa hasara.


4: Angalia gharama ya meza kama unaweza kuimudu, muhimu kabla ya kwenda kununua anza kufanya utafiti wa bei ili ujiandae vizuri.


# KATUNIKA KI'DOMOKRASIA


BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879







*KINYUNYIZO CHA LEO... ...ONDOKA USEMWE

# HABARI KIMATAIFA



Helikopta ya kijeshi ya Marekani, ikiruka karibu na uwanja wa ndege wa Kabul, nchini Afghanistan, ambako siku ya Alhamis kulitokea shambulizi la bomu lililoua askari 13 wa nchi hiyo. **PICHA: DW**

## Marekani yaanza kulipa kisasi shambulio uwanja wa ndege

**KABUL, Afghanistan**

JESHI la Marekani limemuua mtu mmoja anayedaiwa kupanga shambulizi kwenye uwanja wa ndege wa Kabul, nchini Afghanistani, mapema wiki hii.

Operesheni hiyo ya usiku wa kuamkia Jumamosi ilifanywa na ndege zisizo na rubani na ilimlenga mtuhumiwa wa kundi la wanamgambo lenye mafungamano Dola la Kiislamu, IS-K kwenye jimbo la mashariki Nangahar. Msemaji wa Kamandi Kuu ya Marekani, Bill Urban, alisema dalili za awali zinaonesha kuwa wamemuua mlengwa na hakuna raia waliouawa.

Shambulizi hilo limefanyika baada ya Rais Joe Biden, kuapa kupambana na IS baada ya mashambulizi ya Alhamisi yaliyosababisha mauwaji ya wanajeshi 13 wa Marekani na raia 79 wa Afghanistani kujeruhiwa.

IS ilikiri kuhusika na shambulizi hilo, huku kundi la Taliban likikanusha kuhusika kwa namna yoyote.

Biden pia aliliagiza jeshi kufanya mashambulizi dhidi ya viongozi wa IS, pamoja na mali za kundi hilo.

Upande mwingine, Marekani ilisema itaendelea kuwaondoa raia wa Afghanistan kutoka uwanja wa ndege wa Kabul hadi dakika ya mwisho, licha ya kuwapo wasiwasi kuhusu mashambulizi zaidi ya kundi la IS.

Wizara ya Ulinzi ya nchi hiyo, ilisema bado kuna vitisho vya kuaminika katika uwanja huo wa ndege.

Marekani bado inaendelea na mchakato wa kuwaondoa raia wa Afghanistan wanaotaka kuondoka.

Msemaji wa kundi la Taliban, alisema kwamba wamechukua udhibiti wa maeneo ya uwanja wa ndege. Hata hivyo, Marekani imekanusha taarifa hizo.

Kwa mujibu wa Msemaji wa Ikulu ya Marekani, Jen Psaki, wataalamu wa usalama wa taifa wamesema kuna uwezekano wa kutokea shambulizi jingine na siku zijazo zitakuwa hatari zaidi.

Siku ya mwisho ya vikosi vya Marekani kuondoka nchini humo ni Agosti 31.

Nchi nyingi za Jumuia ya Kujihami ya NATO zimemaliza safari zao za dharura za ndege kuwaondoa watu.

Wanajeshi wa Marekani pamoja na washirika wake wamewaondoa watu 12,500 kutoka uwanja wa ndege wa Kabul, katika muda wa saa 24 zilizopita, licha ya operesheni hiyo kuahirishwa kutokana na shambulizi hilo. Ikulu ya nchi hiyo ilisema watu 8,500 waliondolewa moja kwa moja na jeshi la Marekani na wengine 4,000 waliondolewa na ndege za washirika wake.

Wakati huo huo, wanajeshi wote wa Ujerumani pamoja na maofisa waliokuwepo Afghanistan, waliwasili Ujerumani kwa kutumia ndege tatu za kikosi cha anga ambazo zilitua juzi usiku katika uwanja wa ndege wa kijeshi wa Wunstorf karibu na Hanover.

Ndege moja ya jeshi chapa ya Airbus A310 na ndege mbili za usafirishaji chapa A400M zilitumika kuwarudisha Ujerumani wanajeshi hao.

Wanajeshi hao wamerejea nyumbani baada ya kukamilika kwa shughuli ya mwisho ya kuwaondoa nchini Afghanistan.

**DW**

## Marekani yaituhumu China Covid-19

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amesema China bado inaficha taarifa muhimu kuhusu kiini cha ugonjwa wa Covid-19.

Kauli hiyo ni baada ya jumuiya ya kiintelijensia ya Marekani kusema haiamini kama virusi hivyo viliundwa kwa madhumuni ya kuwa silaha ya kibailojia, ingawa bado wamegawanyika kuhusu uwezekano wa kuwa viilitoroka katika maabara.

Hata hivyo, Biden alisema nchi yake itaendelea kushirikiana na washirika wake kuishinikiza serikali ya China kutoa taarifa zaidi pamoja na kushirikiana na Shirika la Afya Ulimwenguni WHO, kwa kusisitiza ulazima kuwapo na uwazi katika kukabiliana na janga.

Marekani haina imani na maofisa wa China, ambao walikuwa na ufahamu wa awali kuhusu virusi hivyo katika hatua zake za mwanzo, kabla ya kuwa na madhara zaidi na kugharimu maisha ya zaidi ya watu milioni 4.5 duniani kote.

**DW**

## Uganda yatibua shambulio la kigaidi

**KAMPALA, Uganda**

SERIKALI ya Uganda imesema imetibua njama ya kufanyika shambulizi la bomu la kujitoa muhanga lililolenga mazishi ya kitaifa ya ofisa mwandamizi wa polisi na kamanda wa jeshi ambae aliongoza mashambulizi dhidi ya wanamgambo wa Al-Shaabab nchini Somalia.

Kikosi cha usalama kilisema jana kwamba siku ya Alhamis kimemkamata mtuhumiwa huyo huko kaskazini mwa mji wa Pader, usiku wa kuamkia siku rasmi ya mazishi ya Meja Jenerali Paul Lokech, ambae kwa jina la utani aliitwa "Simba wa Mogadishu".

Msemaji wa jeshi, Brigedia Flavia Byekwaso, alisema mtuhumiwa huyo ambaye alijitambulisha kama raia wa Uganda kwa jina la Katumba Abdul, alikutwa na nyenzo kadhaa za kivita ikiwamo vifaa vya kutengenezea bomu.

Rais Yoweri Museveni, alishutumu shambulizi hilo, kundi la waasi wa ADF, ambalo kwa mara ya kwanza liliibukia Uganda 1996, lakini katika kipindi hiki limekuwa na nguvu zaidi katika eneo la mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, na kutajwa pia kuwa na mwingiliano na kundi la Dola la Kiislamu.

**DW**

========================

## Rais wa zamani mali atolewa kizuizini

**BAMAKO, Mali**

JUMUIYA ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS), imesema kiongozi wa zamani wa mpito wa Mali, Bah Ndaw na waziri mkuu wake, Moctar Ouane, wameondolewa kizuizi cha nyumbani.

Katika taarifa iliyotolewa na ECOWAS, inaeleza inaikaribisha hatua hiyo ya Mali ya kuwaondolea vizuizi viongozi wote wa zamani na wote wawili wanapaswa kupata fursa na haki zote za kimsingi kama rais na waziri mkuu wa zamani.

Kabla ya kuondolewa madarakani katika mapinduzi ya pili yaliyofanywa na Kanali Assimi Goita, rais huyo wa zamani wa mpito na waziri mkuu wake walichaguliwa kama viongozi wa kiraia baada ya mapinduzi ya kijeshi ya Agosti 2020.

**DW**

## MAKALA



Na Magabilo Masambu

# UTAJIRI WA DUNIA UKO MAKABURINI

NAKUMBUKA miaka ya 1990 nikiwa mdogo kila tulipokuwa tunamaliza kula chakula hasa cha usiku, bibi yangu alikuwa na utamaduni wa kunisimulia hadithi fulani ndefu na katikati ya hadithi hizo aliimba na nyimbo nzuri sana ambazo wakati mwingi zilitumika kunibembeleza nakujikuta napata usingizi mnono.

Hadithi hizi tuliziita kikwetu "amagani", kwa sababu nilikuwa mtoto sikuwa nafahamu hasa zile hadithi zilimaanisha nini, bali nilizifurahia na bibi yangu kwa kweli alikuwa mahiri sana katika eneo la hadithi maana ni hadithi ambazo hazikuwa na mwisho, zilikuwa ni hadithi zenye mwendelezo na nzuri sana kuzisikiliza.

Hii ni kwa sababu maisha yangu ya utoto karibu yote nililelewa na bibi yangu. Nafikiri hadithi zile zaweza kuwa zimenifanya leo nimekuwa mwandishi wa vitabu katika maeneo mengine kwa sababu nilikuwa natumia muda mwingi zaidi kusimuliwa mambo mengi wakati ule nikiwa mdogo japo nilikuwa sijui kusoma na kuandika.

Bibi yangu leo bado yuko hai lakini hana kumbukumbu tena kwa sababu ya umri mkubwa. Kila wakati huwa najaribu kumkumbusha kama anaweza kuzikumbuka ili nipate nafasi ya kuziandika vitabuni lakini hawezi tena. Ni jambo ambalo linaniumiza sana natamani siku zirudi nyuma wakati ule uwe sasa. Haiwezekani tena hakumbuki chochote, natamani niziweke kwenye mfumo wa mazungumzo (video) pengine ningepata tamthilia nzuri sana za kiafrika. Haiwezekani kwani hakumbuki tena!

Wako watu wengi ambao wanazeeka na mwisho kufa na mawazo yao ambayo yangelibaki kama mafunzo makubwa kwa vizazi vyetu. Utajiri wa dunia uko makaburini kwa sababu hatuna utamaduni wa kuhifadhi mawazo katika maandishi au hata katika kumbukumbu nyinginezo. Pengine ni kwa sababu ya mazingira kama ilivyotokea kwangu au kutokana na kutoona umuhimu wa kufanya hivyo.

Angalau siku hizi baadhi ya viongozi na watu wengine wameanza kuwa na utamaduni wa kuandika vitabu wanapostaafu kazi au wanapofikia katika umri wa uzee. Ni jambo jema kwani vitabu hivyo vitabaki na uzoefu, mafanikio yao katika maeneo mengi jambo ambalo litafanya wasomaji kufahamu baadhi ya mambo ambayo yaweza kuwa msaada mkubwa katika maisha yao.

Maandiko yanasema: "Kila nafsi itaonja mauti." Hii ina maana hakuna atakayesalia duniani ni jambo la wakati tu, hivyo tu wasafiri. Lazima kila wakati tujiandae kusafiri kwenda ng'ambo huku tukihakikisha kwamba tunaacha chakula cha familia (vitabu) ili tusiondoke na utajiri wetu kwasababu utajiri wowote unaanza na wazo kisha unapata mali.

"Usomaji wa vitabu baada ya umri fulani, unaongeza fikra kwa kiwango kikubwa na kuboresha uwezo wa kutafakari" (Albert Einstein, 2879-1955). Ni ukweli kwamba kuna tofauti kubwa sana ya mtu anayesoma vitabu na asiyesoma katika kufikiri na kuamua mambo, iwe ni kwenye biashara, kilimo, sheria na hasa kwenye siasa kwa sababu hakuna jambo jipya duniani. Tunachofanya ni kusoma mawazo ya wengine katika jambo fulani waliamuaje wakati huwo na sisi tutafute njia bora ya kuyaamua kutokana na mazingira yetu.

Hatuwezi kupata vitabu kama hapatakuwapo waandishi. Kwa maana hiyo, ni muhimu sana kuweka mawazo yetu au ya watu wetu wa karibu vitabuni ili wasiondoke nayo, maana hakuna siku tutayapata tena wakishaondoka.

Wako watu wanaodhani kwamba ili uandike kitabu inakuhitaji uwe na elimu kubwa sana labda ya digrii hapana kila mtu anaweza kuandika kitabu ilimradi uwe na wazo bora kwaajili ya jamii. Wakati nikiandika kitabu changu cha kwanza, swali la wasomi wengi niliokutana nao, walikuwa wanauliza kiwango changu cha elimu. Jambo la kushangaza ni kwamba wao wenyewe pamoja na kuwa na elimu kubwa zaidi yangu hawajawahi kuandika hata kipande cha gazeti na wanasahau kwamba kuna tofauti kati ya elimu na akili.

Vitabu vilianza kuandikwa kwa mkono kisha baada ya maendeleo ya teknolojia sasa watu wanachapa kutumia kumpyuta hii ina maana hata kama hauna kompyuta bado unaweza kuandika wazo lako kwa mkono kwenye karatasi au daftari kisha kuchapwa baadaye kama kitabu.

Tuwasaidie wale tunaodhani wana mambo mazuri ya kuandikwa bahati mbaya tulio nayo. Tunadhani kwamba mawazo mazuri hutoka kwa viongozi tu na kwamba kama mtu si kiongozi hana nafasi hata ya kuhojiwa. Mfano katika nchi hii, wako watu wanaifahamu historia ya Tanzania, utamaduni wake vyema lakini kwa sababu si maarufu hata kama wanajulikana, hawarekodiwi. Mawazo yao hayaandikwi mwisho wa siku wanakufa na mawazo yao na utajiri huo unafukiwa makaburini.

Kutokana na changamoto ya maisha kubadilika, siku hizi watu wengi wanapenda kuandika na kusoma mambo yanayohusu zaidi biashara tu lakini lazima tutambue kwamba tunaweza kupoteza historia na utamaduni wetu kama Watanzania na waafrika.

Kuna watu wana mawazo mazuri sana ambayo pengine yangewafanya wawe matajiri lakini kwa sababu hayaandikwi, wanakufa wakiwa masikini na kuondoka na utajiri vichwani mwao.

Wito wangu kwa Watanzania wenzangu, tusikubali kuondoka na mawazo yetu wala tusisubiri kuwa wazee au wastaafu ndipo tuandike mawazo yetu. Tutakuwa tumechelewa, wakati ni sasa weka mawazo yako kwenye maandishi tukusome tukufahamu. Lakini zaidi mawazo yako yawe kwa ajili ya faida yako na wengine pia.

***0689157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***
***ARUSHA-TANZANIA***

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO



Na Adam Fungamwango

# *Juma Ubao 'alipobatizwa', 'King Makusa'*

MOJA na vibao vilivyovuma sana mwanzoni mwa miaka ya 1980 ni 'Posa Nitaleta'. Wimbo huu ulipigwa na bendi ya Biashara Jazz ambayo kwanza kabisa ilitumia mtindo wa 'Dundadunda' na baadaye wakajiita 'Kumbakisa'.

Wimbo huo ulitungwa na aliyekuwa kiongozi wa bendi hiyo, Juma Ubao. Awali mwenyewe aliuita 'Mshenga'. kamati ya Uchujaji wa Maadili ya Nyimbo, Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD), wakakataa kuupa wimbo huo jina la 'Mshenga'. Mwenyewe alidai kuambiwa kuwa kuna nyimbo zenye majina hayo nyingi sana ambazo zimerekodiwa. Mbaraka Mwinshehe tayari alishakuwa na nyimbo tatu zinazoitwa 'Mshenga', hivyo akaambiwa abadilishe.

Huko na huko, wimbo huo ukapewa jina la 'Posa Nitaleta'. Ni wimbo ambao kwa mujibu wa mwenyewe Ubao ni kisa cha kweli ambacho kilimtokea na kusababisha atunge.

Anasema alitunga kwa sababu ya hasira iliyosababishwa na rafiki yake huyo ambaye alimwamini, lakini alileta tafrani kubwa ya kusababisha akose mke. Ni rafiki yake ambaye aliishi naye chumba kimoja na alipotaka kuoa akamtumia kama mshenga. Akampa posa kupeleka kwa wakwe. Hata hivyo, baadaye iligundulika kuwa hakupeleka pesa yoyote na alilla. Kwa hasira, Ubao akasema alimpeleka mahakamani. Lakini alipofika huko alikuwa mjanja na kuuliza ushahidi kama kuna maandishi yoyote ya kukabidhiana pesa Hayakuwapo.

Na mahakamani siku zote kinachotakiwa ni ushahidi. Hakukuwa na ushahidi wowote wa watu wala maandishi. Mshenga akashinda kesi. Ubao akasema hiyo ilimuuma mno na kwa sababu ni mwanamuziki, hasira zote akazimalizia kutunga wimbo huo.

Mwenyewe alisema kuwa alimtaja hadi jina mshenga huyo, lakini kwenye kamati ile ya kuchuja, iliiondoa pia jina akaelezwa kuwa lengo si kukomoana au kuchochea ugomvi, bali ni kuifundisha jamii na kuelimisha.

"Kweli, yote hupangwa na Mungu. Nilitaka kuoa, pesa mali nilitoa. Msichana huyu kidogo tulipendana. Hapo mwanzo nilisema fitina za mashemeji. Sasa yamenikuta huyu mchumba wa pili. Ukweli nia nilikuwa nayo ya kwamba, harusi ifanyike. Sijui kitu gani harusi yaikuwa wala pati. Ni kazi ya Mungu oooh hupangwa na Mungu yote. Siku moja nilikwenda kwa wakwe zangu, kupanga sherehe za harusi yangu. Wakwe walisema hatuja pata mali, wala posa, karibu tena mkwe we kalete posa kwanza we, uoe mke.

"Kumbe mshenga hakupeleka posa kwa wakwe, nitafanya nini yeye, ohoo, nilipompa pesa hakuwepo shahidi nitafanya nini yeye, ohoo. Mshenga kapotea, posa na mali, hakupeleka yeye, ohoo.

Mimi nilikwenda polisi kumshitaki mshenga, polisi walisema subiri baba tutafanya uchunguzi wiki hii, kabla wiki haijafika polisi waliniita njoo njoo baba hoo. Mshenga wako kakamatwa ashitakiwe kama mwizi ee. Tulipofika mahakamani eee, mshenga aruka, asema hakupokea pesa. Aliuliza ushahidi uko wapi ee baba ooo, aliuliza maandishi yako wapi Jeni mama subiri. Ai mama nitaleta posa, japo kuwa siyo kizito kwa macho." Hayo ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo.

Huo ndio wimbo uliosababisha Ubao akapachikwa jina la 'King Makusa' na mshabiki wake na wa bendi hiyo. Ni kwa sababu mbali na kuimba wimbo huo, kupanga muziki, alipiga gita la solo, halafu akapiga na kinanda kwa wakati mmoja. Kumbuka kipindi hicho njia ya kurekodi ilikuwa moja, hivyo bendi ilikuwa inarekodi kama iko ukumbini inatumbuiza na si kama sasa, kila chombo kina siku yake ya kuingizwa kwenye mashine.

Wakati wa kuimba, alikuwa akiimba huku akidokoa gita. Wakati wa sebene, alipiga gita, halafu wakati wa kuingia kinanda, kuna ufundi ulifanyika wa kitaalam wa muziki, anaachiwa mpiga saxophone atambae. Lakini lengo ni kwamba Mzee Makusa, avue gita na kwenda kwenye kinanda. Akifika, kwenye sax, anaacha na mzee anaanza kupiga kinanda hadi anamaliza. Anapomaliza, anamwacha tena mpiga sax aingie na kufanya vitu vyake. Lengo ni kumfanya Ubao atoke kwenda kwenye kinanda kwenda kuvaa gita la solo na akaanza kupiga tena. Ni ufundi wa hali ya juu ambapo kama si mwanamuziki wa ukweli unaweza kukosea na wimbo huo ukarekodiwa siku nzima.

Hiyo ilifanyika hata kwenye maonyesho ya bendi hiyo, hivyo mashabiki kwanza wakampachika jina la 'King Makusanya', ikiwa na maana anafanya kazi nyingi kwa wakati mmoja, akivikusanya vyombo vya muziki. Baadaye hao hao mashabiki wakaona jina ni refu sana na hakitamkiki vizuri. Wakaamua kumwita 'King Makusa'. Ndiyo jina ambalo hadi leo limemkaa kama amezaliwa nalo. Huyo ndiyo Juma Ubao 'King Makusa'. Ambaye alipatwa na mkasa mzito uliosababisha atunge wimbo uliompatia jina la kimuziki ambalo limebaki kama nembo yake daima.

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald. Kijana msomi aliyetoka nchini Marekani, anarejea nchini Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya mapenzi-21

**Na Adam Fungamwango**

(0716 350534)




"Hivi we Donald leo umenifuata nyumbani kwangu ukiwa umekunywa?"

"Sijakunywa, ila nawaambia tabia mliolifanya sijaipenda na si nzuri na hivi tu kwa sababu waliofanya hivyo ni baba na mama, vinginevyo saa hizi ningekuwa nimeshalibwaga jambo hili polisi."

Hofu kidogo ilimuondoka Doroth akijua Donald hatoweza kusema jambo lile polisi kwa sababu asingependa wazazi wake wakamatwe.

"Na hili nenda kawaambie wenzio kuwa nimejua."

"Si uende ukawaambie mwenyewe uongo wako wazazi wako."

"Siwaambii, ila siku wakitiwa pingu na wewe mwenyewe ndiyo mtajua."

************************

Koplo Peter aliingia ofisini kwa bosi wake, Inspekta Andrew. Alikuwa ameitwa. Kwa bahati mbaya alikuwa akisikiliza simu. Akasimama kimya.

"Unasemaje?" Sauti ya Inspekta ilisikika ikiongea na mtu aliyekuwa akiongea naye kwenye simu.

"Amekufa?" Akauliza.

"Hujui?" Sekunde chache baadaye akakata simu.

Akashusha pumzi ndefu.

"Afande Peter, hili sakata linaonekana sio la kawaida. Kuna tatizo."

"Kwa nini afande? Aliuliza koplo Peter baada ya kupiga saluti.

"Donald amepata ajali mbaya."

"Imekuwaje afande, amefariki?"

"Na mimi nimeuliza hivyo hivyo?"

"Wanasemaje?"

"Hawajui."

"Nani?"

"Ni kituo cha Polisi Kawe. Ajali imetokea kwenye makutano ya Kawe na Tegeta. Lakini bado wanafuatilia."

Kimya kilitawala kidogo, kila mmoja akitafakari, kabla ya koplo Peter kuvunja kimya hicho.

"Sasa umehusishaje, tukio hili na tukio hili la mauaji?"

"Ndiyo maana sisi ni askari na si raia. Binti anauawa. Watu wanasema kwa ajali, lakini kwenye kichwa chake yakakutwa mabaki ya risasi. Tumewahoji watu kadhaa. Lakini siku mbili tu baada ya kumhoji mpenzi wake naye anapata ajali. Huoni kuna kitu?"

"Ina maana afande unadhani kuwa si ajali ya kawaida?"

"Hata kama ni ya kawaida. Sisi tunatakiwa tudhani hivyo. Na hii itatusaidia kupata ukweli.

Cha kufanya, ni kwamba askari wa kituo cha Kawe, walikuwa wanaelekea eneo la tukio, nimewaambia kama kutakuwa na maiti ya majeruhi wapelekwe kwanza kwenye Hospitali ya Mwananyamala. Wahi kwanza huko, halafu wewe ndiyo utanipa taarifa kamili ya nini kimetokea na kama Donald atakuwa amefariki au la.

> **"Ndiyo fanya hivyo na wote wanaokuja kumtazama wahakikishe wanakaguliwa vizuri, lakini pia wahakikishe wanaingia wawili wawili na wasikae muda mrefu, sawa?"**

"Sawa afande."

*****************************

Haikuwa kawaida yake. Alijihisi mchovu. Hakujua umetokana na nini. Aliendesha gari kivivuvivu. Hali ya hewa ilikuwa ni ya manyunyu ya mvua. Ilikuwa ni majira ya saa 1: 00 usiku. Alikuwa akirejea nyumbani kwao Mbezi Beach. Alipofika karibu na maeneo ya makutano ya Kawe na Tegeta, ghafla aliona bodaboda tatu zilizokuwa zikija mbele yake kwa namna ya kumchanganya. Zilionekana zinaendeshwa na vijana ambao walikuwa mahiri na watundu kwa uendeshaji ule. Ingawa walikuwa wamefuatana, lakini walikuwa wakiyumba barabarani.

Baadaye wa mbele aliinua gurudumu juu na kuendelea kutembea na gurudumu moja la nyuma, lakini kwa namna ambayo alionekana kama amedhamiria kumvaa.

Haikuwa hivyo. Alipowakaribia, wote walilikwepa gari lake kwa namna ya ajabu, lakini kutokana na wasiwasi gari lake liliyumba.

Ghafla likagonga ukingo wa barabara, likapanda juu na kuanguka kwenye mteremko, kabla ya kubingirika mara tatu.

Waliokuja kumchumoa hawakuwa na utaalam wa kujua kama alikuwa hai au amekufa. Ni kwa sababu hakuwa na jeraha lolote, wala kupasuka kichwa. Lakini alikuwa kimya.

Hakuwa mwingine ni Donald.

***********************************

"Afande nimefika hospitali ni kwamba Donald yu hai, lakini. Mpaka sasa hawezi kuongea, kuna wakati alifumbua macho. Cha ajabu aliponiona alitabasamu. Dakika chache baadaye usingizi mzito ukamchukua tena." Koplo Peter alikuwa akiongea na Inspekta kwa simu yake ya mkononi.

"Unajua nia yangu ya kukwambia uwahi? Ni kwamba kama ajali ni ya kupangwa kama atakuwa hai, basi upesi nilitaka ulinzi uimarishwe hapo. Kwa sababu kama ni hivyo tunavyodhani anaweza kuja kumalizwa hapo hapo. Kama uchuguzi itagundua kuwa ni ajali ya kawaida, basi tutafanya kitu kingine."

"Sawa afande basi nitaita maafande wawili wakae hapa kwenye kitanda chache kwa ajili ya ulinzi."

"Ndiyo fanya hivyo na wote wanaokuja kumtazama wahakikishe wanakaguliwa vizuri, lakini pia wahakikishe wanaingia wawili wawili na wasikae muda mrefu, sawa?"

"Sawa afande."

"Sawa, unajua inawezekana ni ajali ya kutengenezwa. Huenda kuna kitu anakifahamu huyu jamaa kuhusiana na mauaji ya mpenzi wake, au wanaona kama vile ameanza kupata fununu, kwa hiyo alindwe kwa gharama yoyote.

******************************

Hali ya Donald ilianza kuimarika baada ya siku nne. Alianza kuwafahamu watu wanaomtembelea hospitalini.

Hata hivyo, alishangazwa na utaratibu aliowekewa wa kuangaliwa kama mgonjwa. Awali alijua utaratibu umebadilika.

Baadaye akagundua ulikuwa ni kwa ajili yake tu. Kwanza kulikuwa na watu ambao walionekana kumlinda. Ingawa hawakuwa wamevaa sare, lakini baadaye aliwagundua kuwa ni askari.

Wao ndiyo walikuwa wakiwakagua wote wanaokwenda kumjulia hali. Na hawakutakiwa kukaa muda mrefu, kabla ya wawili mwingine kuruhusiwa.

Alishangaa ni kwa nini askari waliamua hivyo baada ya kupata ajali.

"Ina maana wameona si ajali ya kawaida nini?"

Wakati akiwaza hivyo, aliona watu wawili wamesimama mbele yake.

Alikuwa ni Doroth na dada yake.

Donald hakupokea kitu chochote kutoka kwao. Bado alikuwa na kinyongo cha kuonekana kuhusika na kifo cha mpenzi wake.

"Vipi, hivi simu yako ilipona kweli?"

"Simu gani?"

"Kwani huna simu wewe?"

"Simu ina maana gani? Mimi si nimepona?"

"Kwa hiyo wewe huna simu hapo. Maana hata nikipiga haipatikani?"

"Doroth, unapigaje simu wakati mimi nimelazwa hospitalini? Unanipigiaje simu?" Kwani kuna nini?"

"He, baba basi, tufanye yameisha."

"Wewe badala ya kuangalia afya ya mgonjwa, unaulizia simu. Kwenye ajali simu inasalimika kweli? Kama haikuharibika, basi vibaka yatakuwa wameichukua."

Doroth na dada yake waliondoka. Na wao walikuwa wa mwisho kumuona mgonjwa.

"Kwani simu ina nini?" Alianza kujiuliza Donald.

Alirudisha akili yake nyuma kabla ya ajali. Anachokumbuka ni kwamba simu yake ilikuwa imeisha chaji.

Akakumbuka kuwa aliiweka kwenye droo ya gari. Mpaka sasa hakujua gari yake imeharibika kiasi gani.

Akakumbuka hajapoteza simu kwenye ajali hiyo, labda tu itakuwa imeharibika baada ya ajali.

Ghafla alipata mgeni ambaye hakutarajia. Haukuwa muda wa kuangalia wagonjwa. Ilishatimu saa mbili usiku. Kila mgonjwa alikuwa kitandani kwake.

*Itaendelea Jumapili*

MECHI KALI

HOME

WOLVERHAMPTON

4.33 | 3.42 | 1.88

MANCHESTER UTD

AWAY

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO



# KANYE WEST AJIWASHA MOTO HADHARANI

RAPA maarufu wa Marekani, Kanye West, amewashangaza mashabiki baada ya kujiwasha moto hadharani wakati wa onesho lake la tatu lililofanyika mjini Chicago.

Tamasha hilo ambalo lilikuwa maalumu kwa ajili ya kutambulisha album yake mpya "Donda", liliwapa mshtuko mashabiki baada ya msanii huyo kujiwasha kibiriti na kisha kuibuka moto mkubwa.

Hata hivyo, baada ya muda mfupi, wasaidizi wake waliuzima, kisha akatokea mwanamke ambaye alivalia shela la harusi wakafunga ndoa na Kanye uwanjani hapo.

Mwanamke huyo ambaye anatajwa kuwa ni Kim Kardashian, licha ya kufikishana mahakamani kwa madai ya talaka lakini bado ameendelea kumuunga mkono Kanye kwenye masuala yake.

# Harmonize azidi kuonyesha uwezo wake

**Na Veronica Ngogona, SAUT**

HATIMAYE mkali wa Bongo Fleva, Rajab Abdul, maarufu kama 'Harmonize', ameachia ngoma mbili mpya kama ishara kwamba hawezi kupoa.

Ngoma hizo zinazoitwa 'Teacher' na 'Kilofeshe' baada ya kuziachia tu, mashabiki wake walijitokeza na kumpatia pongezi kwani itakuwa mara yake ya kwanza kutoa nyimbo mbili kwa mpigo.

Hata hivyo, nyimbo hizo baadhi ya mashairi yake yameonekana kama madongo kwenda kwa aliyekuwa kiongozi wake katika lebo ya WCB, Diamond Platnumz.



LIVE IN PLAY
BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA




# CASEMIRO AJIFUNGA MADRID HADI 2025




**MADRID, Hispania**

KIUNGO wa Real Madrid, Casemiro, amesaini mkataba mpya ambao utamuweka klabuni hapo hadi Juni 2025.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil mkataba wake wa sasa ulikuwa unamalizika mwishoni mwa msimu ujao.

Lakini sasa atabakia hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu kwa miaka mingine miwili baada ya kusaini kuongeza mkataba mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ni mwingine aliyeamua kuongeza mkataba mpya wa kubakia kwa miamba hao wa Hispania, baada ya Karim Benzema na Federico Valverde kufanya hivyo wiki iliyopita.

Casemiro amecheza mechi 288 kwa Madrid tangu alipowasili hapo akitokea Sao Paolo, awali alitua kwa mkopo Januari 2013, na amefunga mabao 30.

Amefurahia kushinda mataji na klabu hiyo; akishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nne, Klabu Bingwa Dunia mara tatu na LaLiga mara nne.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil pia alikuwa sehemu ya kikosi cha Selecao kilichoshinda Kombe la Copa America mwaka 2019.

# *Jesus, Richarlison kumrithi Mbappe*

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain imewaweka kwenye orodha, Richarlison na Gabriel Jesus kwa ajili ya kuziba pengo la Kylian Mbappe anayetajwa kutaka kwenda Real Madrid.

Kwa mujibu wa Jarida la France Football, PSG inaamini kwamba, kuna uwezekano mdogo wa kubamkiza Mbappe kwenye kikosi chake, hasa baada ya msimu huu na hivyo wameamua kuangalia nyota wanaoaweza kuchukua nafasi yake.

Ingawa PSG haina mpango wa kumuuza Mbappe katika dirisha hili la usajili wa kipindi cha majira ya joto, lakini nyota huyo anaweza kuondoka akiwa mchezaji huru msimu ujao.

Licha ya Real Madrid kutoa ofa ya euro milioni 180 kwa ajili ya kutaka kumsajili Mbappe, lakini PSG wamekataa ofa hiyo na kutaka iboreshwe zaidi.

Mapema juzi PSG iliweka wazi ada ya kumuachia Mbappe ya euro milioni 220 na bila hiyo hawatakuwa tayari kumuuza.

Na wakati sakata hilo la usajili likiendelea, PSG sasa imeanza kuangalia wapi ambapo inaweza kupata wachezaji wa kuziba pengo lake.

Kwa mujibu wa televisheni ya Globo Esporte, PSG wanamtaka Jesus kutoka Manchester City ingawa kocha wake, Pep Guardiola amebainisha wazi kwamba hatarajii kuona nyota wake huyo akisepa hapo kwenye dimba la Etihad.

Pia PSG imeonyesha nia ya kumtaka nyota wa Everton na Brazil, Richarlison kwa mujibu wa ESPN Brazil.






## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 29 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 4301 | Utrecht vs Feyenoord | 2.81 | 3.31 | 2.40 |
| 14:00 | 2081 | Troyes vs Monaco | 4.17 | 3.63 | 1.82 |
| 14:00 | 5434 | Rangers vs Celtic | 2.56 | 3.30 | 2.61 |
| 14:30 | 5961 | KAA Gent vs Brugge | 3.15 | 3.20 | 2.25 |
| 15:15 | 1526 | FC Luzern vs Lausanne-Sport | 1.82 | 3.75 | 3.85 |
| 15:30 | 1562 | Heracles Almelo vs NEC Nijmegen | 1.78 | 3.84 | 3.94 |
| 15:30 | 2192 | Ajax vs Vitesse Arnhem | 1.20 | 6.69 | 10.82 |
| 16:00 | 1780 | Burnley vs Leeds | 2.97 | 3.42 | 2.35 |
| 16:00 | 2497 | Sirius FK vs Djurgardens IF | 4.36 | 3.87 | 1.65 |
| 16:00 | 3566 | Clermont Foot vs Metz | 1.77 | 3.59 | 4.49 |
| 16:00 | 3643 | Angers vs Rennes | 2.89 | 3.14 | 2.49 |
| 16:00 | 5064 | Tottenham vs Watford | 1.45 | 4.52 | 7.03 |
| 16:00 | 5118 | Strasbourg vs Brest | 1.98 | 3.34 | 3.83 |
| 16:00 | 5268 | Lens vs Lorient | 1.74 | 3.68 | 4.57 |
| 16:00 | 5375 | BK Hacken vs IFK Goteborg | 2.14 | 3.10 | 3.29 |
| 16:30 | 1254 | Union Berlin vs Monchengladbach | 2.49 | 3.29 | 2.79 |
| 17:00 | 1297 | Vejle BK vs Copenhagen | 5.31 | 4.13 | 1.55 |
| 17:00 | 1731 | St Mirren vs St Johnstone | 2.87 | 2.97 | 2.57 |
| 17:00 | 2004 | Aberdeen vs Ross County | 1.68 | 3.53 | 5.10 |
| 17:00 | 4941 | FC Minaj vs Shakhtar Donetsk | 14.50 | 6.38 | 1.15 |
| 17:30 | 3999 | FC Basel vs BSC Young Boys | 2.66 | 3.60 | 2.37 |
| 17:30 | 4932 | Grasshoppers vs Servette Geneva | 2.81 | 3.45 | 2.33 |
| 17:45 | 5290 | Heerenveen vs AZ Alkmaar | 3.70 | 3.50 | 1.92 |
| 18:00 | 1225 | Barcelona vs Getafe | 1.46 | 4.52 | 6.77 |
| 18:00 | 1787 | Bohemians FC vs Shamrock Rovers | 3.20 | 3.20 | 2.13 |
| 18:00 | 2539 | Lille vs Montpellier | 1.71 | 3.83 | 4.57 |
| 18:30 | 1053 | Wolverhampton vs Manchester Utd | 4.33 | 3.42 | 1.88 |
| 18:30 | 1081 | Hammarby vs Malmo | 3.25 | 3.54 | 1.98 |
| 18:30 | 2200 | VfL Wolfsburg vs RB Leipzig | 3.39 | 3.49 | 2.07 |
| 18:30 | 4697 | Kalmar vs Elfsborg | 2.57 | 3.10 | 2.61 |
| 19:00 | 5187 | Viking vs Rosenborg | 2.58 | 3.42 | 2.53 |
| 19:15 | 1217 | Kasimpasa vs Galatasaray | 4.35 | 3.75 | 1.73 |
| 19:15 | 3247 | Sivasspor vs Goeztepe | 2.03 | 3.31 | 3.56 |
| 19:30 | 1134 | Racing Genk vs Anderlecht | 2.22 | 3.20 | 3.20 |
| 19:30 | 4980 | Genoa vs Napoli | 5.60 | 4.40 | 1.54 |
| 19:30 | 5995 | Sassuolo vs Sampdoria | 2.03 | 3.72 | 3.41 |
| 19:55 | 4056 | Cukaricki St vs Red Star Belgrade | 5.40 | 4.15 | 1.50 |
| 19:55 | 4999 | NK Osijek vs Dinamo Zagreb | 2.99 | 3.13 | 2.27 |
| 20:00 | 2640 | Sporting Braga vs Vitoria Guimaraes | 1.68 | 3.79 | 4.62 |
| 20:00 | 3815 | Benfica vs Tondela | 1.17 | 6.70 | 13.79 |
| 20:00 | 5437 | MFK Karvina vs Slavia Prague | 7.21 | 4.70 | 1.41 |
| 20:30 | 4387 | Rayo Vallecano vs Granada | 2.56 | 3.17 | 2.86 |
| 20:30 | 5714 | Cadiz CF vs Osasuna | 3.12 | 3.02 | 2.48 |
| 21:00 | 4632 | Brondby vs Midtjylland | 3.45 | 3.41 | 2.03 |
| 21:45 | 1496 | Reims vs Paris St Germain | 12.25 | 6.65 | 1.20 |
| 21:45 | 4191 | AC Milan vs Cagliari | 1.48 | 4.62 | 6.22 |
| 21:45 | 4739 | Salernitana vs Roma | 5.21 | 4.31 | 1.58 |
| 21:45 | 5010 | Altay vs Fenerbahce | 3.10 | 3.44 | 2.16 |
| 21:45 | 5923 | Giresunspor vs Trabzonspor | 4.64 | 3.85 | 1.67 |
| 23:00 | 2635 | Atletico Madrid vs Villarreal | 1.80 | 3.42 | 4.83 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# UNITED ILIVYOIZIDI KETE CITY KUMNASA RONALDO

## Tangazo la miamba hiyo ya kumsajili lilikuja saa 24 baada ya majirani zao kuripotiwa...

**MANCHESTER, ENGLAND**

MANCHESTER United imethibitisha kwamba, imefikia makubaliano ya kumsajili Cristiano Ronaldo kutoka Juventus.

United imekubali kulipa dola milioni 30 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, ambaye jana alitarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya kabla ya kukamilisha taratibu nyingine.

Ronaldo amerudi Man United baada ya kipindi cha miaka 12 tangu alipoondoka hapo na kwenda Hispania.

Ronaldo alifunga mabao 118 katika mechi 292 katika kipindi chake cha kwanza hapo Old Trafford kabla ya kuondoka kwenda Real Madrid mwaka 2009.

"Kila mmoja klabuni hapo anasubiri kwa hamu kumkaribisha Cristiano akirudi Manchester," ilisema taarifa ya klabu hiyo ikinukuliwa na BBC Sport.

Tangazo la United kumsajili Ronaldo lilikuja saa 24 baada ya awali kuripotiwa kwamba, majirani zao Manchester City walikuwa kwenye nafasi nzuri ya kumsajili mshambuliaji huyo raia wa Ureno na kwamba, tayari walikuwa wameshafikia makubaliano ya maslahi binafsi.

Hata hivyo, Ronaldo ameamua kurudi United ambako alitumia miaka sita na kushinda mataji matatu ya Ligi Kuu England, na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la Ligi mara mbili na FA mara moja pamoja na Klabu Bingwa Dunia ya Fifa na Ngao ya Jamii chini ya kocha Sir Alex Ferguson.

Awali, ilionekana kwamba, Ronaldo hangekuwa na nafasi ya kurudi katika klabu yake hiyo ya zamani, lakini United ikaamua kubadilisha gia angani na kumsajili nyota huyo.

Man City walikuwa na nafasi kubwa ya kumsajili hasa baada ya kumkosa Harry Kane ambaye ameamua kubaki katika klabu yake ya Tottenham Hotspur.

Akizungumza kabla ya Man City kuivaa Arsenal kwenye mchezo wa Ligi Kuu jana, Jumamosi, kocha Pep Guardiola alisema: "Cristiano ni mchezaji wa Juventus. Siwezi kuzungumza chochote hapa.

"Zimebaki siku tatu dirisha la usajili kufungwa, chochote kinaweza kutokea, kuna wachezaji wachache akiwamo Cristiano Ronaldo wanaweza kuamua wapi kwa kwenda, Messi tayari ameshafanya uamuzi."

## ZISIKUPITE

### RICHARLISON AWANIWA PSG
KLABU ya Paris St-Germain itajaribu kumsajili mshambuliaji wa Everton na Brazil, Richarlison mwenye umri wa miaka 24, ikiwa watakubaliana kuhusu mpango wa kumuuza mshindi wa Kombe la Dunia wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye miaka 22, kwenda Real Madrid. ***(Sky Sports)***

### EVERTON KUMUUZA NYOTA WAKE
EVERTON wanataka pauni milioni 85 ili kumuachia Richarlison, ambaye ni mchezaji wa zamani wa Watford, mwenye umri wa miaka 24.***(Star)***

### JESUS KUMRITHI MBAPPE
KLABU ya PSG itamlenga straika wa Manchester City na Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 24, ili kuziba pengo la Kylian Mbappe anayetaka kuondoka. ***(Sun)***

### HAALAND KWENYE RADA
MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, ni mwingine ambaye yupo kwenye rada ya PSG endapo Kylian Mbappe atahamia mji mkuu wa Hispania, Madrid. ***(Star)***

### EDOUARD AJADILIWA
EVERTON wamewasiliana na Celtic juu ya uwezekano wa kufikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 23. ***(Sky Sports)***

### CAVANI KUBAKI OLD TRAFFORD
MSHAMBULIAJI wa Uruguay na Manchester United, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34, "bado yuko kwenye mipango ya United msimu huu" na "hakuna mpango wa kumuuza" baada ya kuwasili kwa Cristiano Ronaldo.***(Goal)***

### FERGUSON KAMSHAWISHI RONALDO
KOCHA wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson, alichukua jukumu kubwa kumshawishi mshambuliaji wa Ureno na Juventus, Crisitiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, kurudi Old Trafford ikiwa ni miaka 12 baada ya kuondoka kwenda Real Madrid. ***(Mirror)***

### ZOUMA BADO HAKIELEWEKI
UHAMISHO wa Kurt Zouma wa pauni milioni 25 kwenda West Ham kutoka Chelsea upo mashakani kwa beki huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26. ***(Mirror)***

### CHELSEA YACHELEWA KWA KOUNDE
SEVILLA imesema Chelsea wanapitwa na muda wa kumsajili beki wao raia wa Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22, ambaye ana kifungu cha kuruhusiwa kuondoka cha pauni milioni 77.1. ***(Football-Espana)***

### NYOTA CHELSEA KUUZWA
CHELSEA itawauza Ross Barkley mwenye umri wa miaka 27 na Danny Drinkwater mwenye miaka 31, ili kupunguza mzigo wa kuwalipa mshahara kabla ya tarehe ya mwisho ya uhamisho wa majira haya ya joto Jumanne ijayo. ***(Sun)***

### VILLA INAMTAKA WITSEL
KLABU ya Aston Villa ina nia ya kutaka kumsajili kiungo wa Ubelgiji na Dortmund, Axel Witsel mwenye umri wa miaka 32. ***(Tuttosport)***

HABARI MICHEZO

# TSSAA yageukia michezo MUHAS

Na Saada Akida

TAASISI ya kusaidia wanafunzi kwenda kusoma nje ya nchi, (TSSAA), imegawa vifaa vya michezo vyenye thamani ya Sh.milioni mbili kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) kwa lengo la kuendeleza michezo nchini.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mkurugenzi wa TSSAA, Aloyce Mkwizu, alisema wamegawa vifaa vya michezo ambavyo ni mipira ya wavu na miguu sambamba na jezi.

Alisema mbali na wanafunzi kusoma kozi mbalimbali za afya pia wanaamini michezo ni sehemu kuimarisha afya zao.

**“Serikali kwa sasa imekuwa ikitoa kipaumbele katika kukuza na kuendeleza michezo kwetu TSSAA, tumekuja MUHAS kugawa vifaa hivi, tukitambua katika chuo hiki mbali na kusoma kuna watu wana vipaji vya michezo mbalimbali ikiwamo soka,” alisema Mkwizu.**

Rais wa Serikali ya Wanafunzi MUHAS, Nyiga Kalyango, alisema kupata vifaa hivyo kutawasukuma kushiriki katika michezo mbalimbali na hatimaye kwenda kushiriki mashindano mbalimbali.

Alisema kwa upande wao suala la michezo lilikuwa chini na haikuwa kipaumbele kwao kwa sababu ya ukosefu wa vifaa husika lakini sasa wamepata msukumo mpya baada ya kuvipata.

“Vifaa vimekuja wakati mwafaka, mbali na kozi mbalimbali tunazopata hapa chuo, lakini kuna watu wenye vipaji vya kucheza michezo ikiwamo soka, ‘basketball’ na mingine ila tulishindwa kwenda kushiriki kutokana na ukosefu wa vifaa,” alisema Kalyango.

# MTIBWA YACHOMOA WA KIMATAIFA NAMUNGO FC

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Mtibwa Sugar kwa mara ya kwanza imeweka rekodi ya kusajili mchezaji kutoka nje ya nchi baada ya kuinasa saini ya kiungo mshambuliaji, Nzigamasabo Steve raia wa Burundi, akitokea klabu ya Namungo FC.

Mtibwa Sugar, iliyoanzishwa mwaka 1988, na kuwa mabingwa wa Tanzania Bara mwaka 1999 na 2000, ilikuwa haijawahi kusajili mchezaji yeyote kutoka nje ya nchi, hivyo Nzigamasabo anakuwa mchezaji wa kwanza wa kimataifa kusajiliwa na klabu hiyo.

Mwenyekiti wa klabu hiyo Nassor Aboubakar, alisema kuwa Mrundi huyo ni mmoja kati ya wachezaji waliosajiliwa kwa msimu ujao wa Ligi Kuu.

Aliwataja wachezaji wengine kuwa ni Said Hamisi Ndemla na Ibrahim Ame kutoka Simba ambao wamepelekwa kwa mkopo, George Chota kutoka Mbeya City, beki wa zamani wa klabu ya Simba, Hassan Banda ambaye baadaye alikwenda kucheza soka la kulipwa Afrika Kusini na Hassan Kibailo kutoka Coastal Union.

“Maandalizi yanakwenda vizuri, safari hii tumesajili kwa umakini zaidi kwa sababu tunataka kurejea kwenye nafasi zetu za juu kama ilivyokuwa huko mwanzo,” alisema.

Kuhusu kocha, mwenyekiti huyo alisema kuwa wameingia mkataba na aliyewahi kuwa kocha wa timu hiyo, Thierry Hitimana.

“Tunamshukuru mwalimu Mohamed Badru, tulimchukua ili kutusaidia timu isishuke na kweli lengo ametimiza, lakini sasa tumemchukua Hitimana, alishawahi kuifundisha timu yetu,” alisema.

Mtibwa imeamua kujiimarisha kwa msimu ujao, baada ya misimu mitatu ya tabu na mashaka, ikinusurika dakika za mwisho kushuka daraja.

Hitimana aliachana na klabu hiyo mwishoni mwa msimu uliomalizika zikiwa zimesalia mechi chache kabla ya ligi hiyo kufikia ukingoni kwa kile alichodai ni kutokuwa na maelewano mazuri na wasaidizi wake katika benchi la ufundi.

Hata hivyo, timu hiyo ilimwajiri Badru ambaye aliinusuru kushuka daraja baada ya kuponea mechi ya mchujo (play off) dhidi kwa kuitoa Transit Camp.

FUNDI...



Kiungo wa Simba, Msenegal Pape Ousmane Sakho, akiwatoka wachezaji wa Olympique Club de Khouribga ya Morocco wakati timu hizo zilipocheza mechi ya kirafiki nchini humo Alhamisi wiki hii. **PICHA: SIMBA**

# Dodoma Jiji FC yajichimbia kambini Moro

Na Adam Fungamwango

KIKOSI cha wachezaji 20 cha Dodoma Jiji FC, kimeanza ramsi kambi yake ya kujiandaa na msimu mpya wa mashindano mbalimbali msimu ujao ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA, mjini Morogoro.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Uhusiano wa klabu hiyo, Moses Mpunga, amemwambia mwandishi wetu kuwa kikosi hicho kilianza kambi rasmi na mazoezi juzi, Ijumaa asubuhi, kwenye uwanja wa Chuo cha Ualimu Morogoro, na kitakaa hapo kwa muda wa siku 10.

“Tumeanza rasmi kambi na mazoezi kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano yote tutakayocheza. Tuko kwenye Uwanja wa Chuo cha Ualimu Morogoro na wachezaji waliowasili hapa ni 20, ingawa kikosi kitaongezeka mpaka kufikia wachezaji 27 ambao ndiyo lengo letu tuwe nao kwa msimu ujao,” alisema Mpunga.

Alisema siku za kupiga kambi zinaweza kuongezeka mpaka 14 kulingana na mazingira yatakayokuwapo.

“Tunaweza kutoka siku 10 hadi 14 kutokana na mazingira. Kuhusu usajili mpaka sasa tumesajili wachezaji wanne, na lengo letu ni kusajili wachezaj watano mpaka wanane, kwa hiyo mpaka sasa tunaendelea kusajili, nadhani mpaka siku ya mwisho tutakuwa tumeshatimiza idadi,” alisema mkurugenzi huyo wa mambo ya habari.


Dodoma Jiji, ambayo ilipanda Ligi Kuu na kuanza kucheza kwa mara ya kwanza msimu uliopita, imeacha wachezaji tisa mpaka sasa kwa mujibu Mpunga.

Wachezaji ambao mpaka sasa wametia wino kuichezea klabu hiyo msimu ujao ni Emmanuel Martin na Richard Olomi kutoka Ruvu Shooting, golikipa Mohamed Yusuph kutoka Polisi Tanzania na Aboubakar Ngalema.

# Michezo

Jumapili Agosti 29, 2021

Nipashe


United ilivyoizidi kete City kumnasa Ronaldo

HABARI UK 22

## Mabingwa wa CAF kukipiga Simba Day

**Na Saada Akida**

HUKU kikosi cha Simba kikitarajiwa kurejea nchini leo mchana kikitokea Morocco kilipokuwa kimeweka kambi kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa, Siku ya Tamasha la Simba (Simba Day) Septemba 19, mwaka huu, kitashusha Mabingwa Afrika kucheza nao mechi ya kirafiki, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Habari wa Simba, Ezekiel Kamwaga, alisema baada ya kurejea nchini, wachezaji watapewa mapumziko ya siku mbili na Jumanne wataingia kambini kwa ajili ya maandalizi mengine ya msimu mpya 'Pre Season'.

Alisema kikosi kitaondoka Dar es Salaam na kwenda moja ya mkoa uliokuwa tulivu na mazingira mazuri kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya msimu mpya kwa kucheza mechi za kirafiki na timu za Ligi Daraja la Kwanza na zile zinazoshiriki Ligi Kuu.

"Ni wapi tutaenda kuweka kambi, hilo litawekwa wazi baadaye, ila Jumanne wachezaji ambao hawako katika majukumu ya timu ya taifa, wataingia kambini na kujiandaa kwa ajili msimu mpya," alisema Kamwaga.

Hata hivyo, Kamwaga alipoulizwa kuhusu mechi ya kirafiki ya kimataifa watakayocheza Simba Day Septemba 19, mwaka huu, alisema ipo kamati inayoshughulikia na bado hajafikishiwa mezani kwake na akiipata ataiweka hadharani.

Lakini chanzo chetu ndani ya kamati hiyo, kilitueleza kwamba wanatarajia kucheza na timu moja kubwa iliyowahi kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tutacheza na timu moja kubwa iliyowahi kutwaa Ligi ya Mabingwa Afrika, siwezi kuitaja kwa sababu ndiyo kwanza tupo kwenye mazungumzo, lakini pia Simba ina utaratibu wake wa kutoa taarifa si kila mmoja anaruhusiwa kuzungumza, mtafute Kamwaga atakueleza kama limeshamfikia," kilisema.

Tayari Simba imecheza mechi mbili za kirafiki ikiwa kambini nchini Morocco dhidi ya FAR Rabat iliyomalizika kwa sare ya mabao 2-1 na kisha kutoka kufungana bao 1-1 dhidi ya Olympique Club de Khouribga.

KAWASILI...



Mwanamuziki kutoka DRC Kongo, Koffi Olomide, akiwasili Uwanja wa Julius Nyerere, Dar es Salaam jana mchana, tayari kwa ajili ya kutoa burudani Siku ya Kilele cha Mwananchi, itakayofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa leo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# YANGA KUSIMAMISHA NCHI LEO KWA MKAPA

## ●●● Yasema ni zaidi ya mtoko na burudani, milango kufunguliwa kuanzia saa tatu asubuhi, nyota watua...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kilele cha Siku ya Mwananchi kikihitimishwa leo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, uongozi wa Klabu ya Yanga umesema tamasha hilo si la kukosa kwa sababu ni zaidi ya 'mtoko' kwa wapenzi wote wa soka na burudani nchini.

Yanga leo inahitimisha Wiki ya Mwanachi baada ya shughuli mbalimbali za kijamii zilizofanyika kupitia wanachama, mashabiki na viongozi wa klabu hiyo kote nchini kwa muda wa wiki nzima, ambapo watalitumia tamasha hilo kutambulisha wachezaji wa msimu mpya kuelekea msimu wa 2021/22.

Mbali na utambulisho huo wa wachezaji, pia kutakuwa na burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali wakiongozwa na mwanamuzi nguli na mkongwe wa muziki wa dansi kutoka DRC Kongo, Koffi Olomide, ambaye alitua Uwanja wa Julius Nyerere, Dar es Salaam jana mchana na kupokewa na Msemaji wa Klabu ya Yanga, Haji Manara sambamba na mashabiki wa timu hiyo.

**Mbali na Koffi, Mkuu wa Idara ya Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, alimwambia mwandishi wetu katika jukwaa la burudani watakaowapagawisha mashabiki kwa muziki ni pamoja na Shilole 'Shishi Baby', Chege Chigunda, Mh . Temba, Juma Nature a.k.a Kiroboto, Mzee wa Bwax na wengineo wengi.**

Bumbuli alisema maandalizi yote yamekamilika na kuwataka Wananchi kuhudhuria kwa wingi ili kushuhudia utambulisho huo, lakini pia kupata burudani ambayo anaamini hakuna atakayejutia kiingilio chake.

"Maandalizi yoye yamekamilika na milango kesho (leo), itakuwa wazi kuanzia saa tatu asubuhi, hivyo wanachama na mashabiki wa Yanga, lakini na Watanzania wote kwa ujumla waje kwa wingi bila kukosa, kushuhudia tukio hili kubwa," alisema.

Aidha, alisema baada ya shughuli nzima ya utambulisho na burudani ya kukata na shoka kutoka kwa wasanii hao, mashabiki watashuhudia mechi kali dhidi ya Zanaco ya Zambia ambayo tayari imeshawasili Dar es Salaam tangu juzi.

Kuhusu wachezaji waliokuwa wamebaki nchini Morocco, Bumbuli alisema: "Wote wameshawasili na watakuwapo uwanjani kesho, hivyo mashabiki waje kwa wingi kuwashuhudia katika Kilele cha Mwananchi".

Katika mechi hiyo, pia mashabiki watapata fursa ya kushuhudia nyota wapya wa kikosi hicho wakiichezea timu yao kwa mara ya kwanza kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Bara utakaofunguliwa rasmi Septemba 25, mwaka huu kwa mchezo wa Ngao ya Jamii kati ya Yanga na Simba huku ligi hiyo ikianza siku nne baadaye.

Baada ya tamasha hilo, Yanga itarejea kambini Kigamboni kuendelea kujiandaa kwa mchezo mgumu wa awali wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Rivers United ya Nigeria, utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa kati ya Septemba 10-12, mwaka huu kabla ya kurudiana ugenini baada ya wiki mbili.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042